# Mwongozo kwa Waalimu

## Wakati na Biblia Daraja la tatu na la nne

Mfululizo wa A

Masomo ya saba hadi kumi na mbili

www.besweb.com

## Bible Educational Services

Registered Charity UK (No 1186004)
Imesajiliwa kama shirika la Hisani Uingereza (Namba 1186004)

**Dhamira**
Kuandaa masomo ya Biblia kwa ajili ya wadau ili kutumika kuwakilisha kweli ya Yesu Kristo kwa kizazi kijacho ulimwenguni kote.

**Maono**
Kufikia kizazi kijacho kwa lugha zao kwa kutumia mtaala wetu kamili kwa kukuza na kusaidia mtandao wa kimataifa wa wabia wanaojitolea.

## HABARI KWA UJUMLA

**Bible Educational Services hufanya nini:**

Bible Educational Services (BES) huchapisha masomo ya Biblia ya "Wakati na Biblia/Bibletime", "Maisha Mapya/New Life" na "Wakusanyaji/Gleaners" kwa Lugha ya Kiingereza na kusaidia vituo vya Shule ya Biblia kwa njia ya Posta pamoja na mashirika mengine ya namna hiyo yanayotumia masomo ya BES huko Uingereza na nchi zingine. BES hufanya hivi kwa kutembelea, kutoa ushauri, kutoa mafunzo na kuunganisha mashirika haya na mengine. Sasa hivi, BES inafanya kazi na vikundi mbalimbali kutoka nchi zingine, vinavyohusika na kutafsiri, kubuni, kuchapisha na kusambaza masomo. Masomo haya yanatolewa bure kabisa kwa kila mtoto.

Kwa mara ya kwanza, masomo ya Wakati na Biblia yalitumika huko Kusini mwa Ireland (Uingereza) miaka sitini iliyopita. Bible Educational Services (BES) wamechukua jukumu la uhariri wa masomo ya Wakati na Biblia kwa lugha ya Kiingereza na Lugha zingine. Kwa muda mrefu, Masomo ya Wakati na Biblia (Bibletime) yalichapishwa kwenye muundo wa A4 ambao uliwawezesha wanafunzi kutoka baadhi ya maeneo kutuma masomo yao kwenye kituo cha BES kwa ajili ya kusahihishwa kila baada ya wiki nne. Hivi karibuni, masomo ya miezi sita yamechapishwa kwa muundo wa A5. Muundo huu umefanya utumiaji wa masomo haya uwe rahisi na wakufaa zaidi kwa makanisa na shule ambazo hazina ufanisi mzuri wa mfumo wa njia ya posta. Tunawashukuru Every Home Crusade au Revival Movement huko Belfast Uingereza kwa kutuwezesha kufanya hivi.

Masomo ya BES ni ya kipekee kwa sababu yameandaliwa na vikundi mbalimbali kutoka makanisa na shule mbalimbali ambavyo vimezingatia mtaala (Syllabus). Masomo yamepangiliwa vizuri na yanamruhusu mwanafunzi kuyatumia kwa muda mrefu hadi atakapotimiza umri wa miaka ishirini. Masomo yanapatikana katika madaraja matano ambayo yamezingatia umri tofauti. Nayo ni, masomo kwa ajili ya watoto wa chekechea (chini ya miaka mitano), miaka mitano hadi saba, miaka nane hadi kumi, miaka kumi na moja hadi kumi na mitatu na miaka kumi na minne hadi kumi na sita. Kuna Mtaala wa miaka mitatu katika kila kikundi cha umri (angalia ukurasa wa 6). Vikundi hivi vya umri vinaweza kutofautiana kulingana na uwezo tofauti wa watoto. Rasilimali na masomo ya Wakati na Biblia yanawapa watoto fursa ya kujifunza Neno la Mungu, kujifunza Habari za Biblia na kujifunza kukabiliana na changamoto zinazotokea maishani mwao kulingana na mwongonzo wa Injili ya Bwana Yesu Kristo.

Nakala zilizochapishwa za masomo kwa Lugha ya Kiingereza zinapatikana kwenye tovuti ya BES /BES website – www.besweb.com au kwa katibu ofisi ya BES Uingereza. Yanapatikana pia kwa lugha zingine kwenye tovuti. Kwenye tovuti kuna nyaraka muhimu kwa mtu yeyote au shirika linalopenda kushirikiana nasi.

## Anuani za mawasiliano za BES

**Ofisi ya Uingereza (Northern Ireland) (Mhifadhi wa masomo yote ya Kiingereza)**
37a Belmore Street, Enniskillen, Northern Ireland BT74 6AA
Simu: +44 286 632 2462

**Katibu wa Uingereza**
Bw. Stephen Gillham,
Barua pepe: stephen.gillham@besweb.com

Tovuti: www.besweb.com
Barua pepe: info@besweb.com

**Mshirika Tanzania (Tanzania Partner)**
World Vision Tanzania
S.L.P. 6070 Arusha, Tanzania
Barua Pepe ya Mawasiliano: david_ombeni@wvi.org
Simu: +255 687 231 757

## MWONGOZO kwa WAALIMU

Mwanzoni, masomo ya Wakati na Biblia yaliandaliwa ili yatumike kwa njia ya posta kukiwepo na kituo cha Shule ya Biblia kwa njia ya posta. Sasa hivi, masomo yanaendelea kutumika kwa wingi hata kwenye sehemu ambazo hazina ufanisi wa kutumia mfumo wa posta au hakuna kabisa mfumo wa posta hasa katika makanisa na shule zilizopo Afrika, India na maeneo mengine. Mwongozo wa kufundisha umeandaliwa kwa wale wanaotumia masomo ya Wakati na Biblia katika hali kama hizo. Mwongozo wa kufundisha katika kitabu hiki umeandaliwa kutumika kwa masomo ya daraja la tatu na la nne kwa watoto wenye umri wa wastani wa miaka 11-16.

Kila Mwongozo wa kufundisha hufuata vifungu vile vile vya Biblia vilivyopo katika somo la Wakati na Biblia. Masomo ya Wakati na Biblia na Mwongozo vimeandaliwa vitumike kwa kila wiki. Masomo ya mwezi Aprili yanahusu Pasaka na masomo ya mwezi Desemba yanahusu Krismasi.

Baadhi ya sehemu watakuwa wanatumia masomo yaliyo katika toleo la A4 la kila wiki na wengine watakuwa wanatumia kitabu cha A5 chenye masomo 24 ndani yake. Kwa kawaida, mwalimu au kiongozi hutoa somo la mwezi toleo la A4 na kila wiki sehemu ya kazi hujazwa kanisani au shuleni au hupelekwa nyumbani na kurejeshwa wiki inayofuatia. Mwishoni mwa mwezi, mwalimu au kiongozi hukusanya somo na kwenda kusahihisha kama inavyotakiwa na kumrudishia mwanafunzi/mtoto kazi iliyosahihishwa mapema iwezekanavyo.

Unapotumia kitabu, mwisho wa kila kipindi, vitabu hukusanywa na kusahihishwa. Tumegundua katika sehemu nyingi kuwa, hili haliwezekani. Hivyo basi, pale darasani masomo yanaweza kugawanywa kwa wanafunzi wengine na mwalimu au kiongozi ataongoza usahihishaji wa somo na wanafunzi watasahihisha masomo ya rafiki zao na kutoa maksi. Nyuma ya kitabu kuna sehemu kwa ajili ya kuweka maksi ya kila somo la mwezi na pia mahali pa maoni kuhusu maendeleo ya mwanafunzi. Pia kuna cheti ambacho mwanafunzi anaweza kupewa kinachoonesha asilimia ya alama ambazo mwanafunzi amepata kwa masomo ya miezi sita.

## MAANDALIZI KWA WAALIMU

Hatupendi kutoa shinikizo na kutokuwapa waalimu fursa ya kufanya mambo kwa njia zao wenyewe kulingana na mawazo na mipango yao wenyewe. Haya ni mapendekezo yanayoweza kutumika kwenye utumiaji wa masomo ya Wakati na Biblia.

- **Elewa habari vizuri –** Waalimu wanapaswa kuelewa habari ya Biblia vizuri kwa kadri iwezekanavyo na vile vile somo la Wakati na Biblia linaloendana na habari hiyo ya Biblia. Ni jambo zuri kwa mwalimu kukamilisha somo la Wakati na Biblia kabla ya kipindi. Mwongozo wa kila somo unapaswa kutumiwa kwa umakini kama chombo cha kumsaidia mwalimu anapojiandaa kwa ajili ya somo.
- **Elewa funzo ambalo watoto wanastahili kupata au kujifunza –** Juu ya kila mpangilio wa somo utaona maneno ‘Tunajifunza kuwa’ ikifuatiwa na makusudio mawili ya kujifunza ambayo tunatumaini kwamba watoto watayaelewa baada ya kumsikiliza mwalimu akifundisha na kukamilisha somo la Wakati na Biblia. Kusudio la kwanza la kujifunza linahusu ufahamu wa habari na la pili linamtia moyo mtoto kufikiri juu ya ufahamu huo, kuutumia na kuuitikia. Makusudio haya ya kujifunza ni sentensi kamilifu na fupi ya mawazo au kweli kuu zinazofundishwa katika somo. Waalimu wanaweza kuzitumia kwa ajili ya tathimini zao binafsi za ufundishaji na mafunzo ambayo watoto wamepata.
- **Toa Utangulizi –** Kwa masomo yote, tunaanzia mahali ambapo watoto wapo katika uzoefu wao wa hali husika. Tumependekeza njia kadhaa ambazo zinaweza kutumika kufanya utangulizi wa habari ili kuwawezesha watoto kuhusika katika kujadili mwanzo wa habari.
- **Fundisha –** Tumetoa dondoo muhimu katika habari. Tunaamini kwamba waalimu hawatazinukuu wakati wanafundisha habari lakini watakuwa na uelewa mzuri wa habari na wataweza kuifundisha katika njia inayofurahisha na kusisimua. Mwalimu atahitaji watoto waelewe mafunzo muhimu kutoka kwenye habari na kuwasaidia kuuelewa mwitikio watakaoupata kutoka kwenye habari waliyojifunza. Kwa usahihi, tumejaribu kuweka pamoja baadhi ya maelezo kwa ajili ya kufundisha habari. Haya yameandikwa katika maandishi *YA MCHALAZO (Italics)*.
- **Kuonesha –** Tunatambua kuwa katika baadhi ya mazingira, sio rahisi kupata vielelezo au video. Lakini, ni muhimu kadri iwezekanavyo kuwa na picha au vitu vinavyoweza kuwasaidia watoto kuielewa habari vizuri zaidi. Vielelezo vitakuwa muhimu sana wakati ambapo mwalimu anaelezea habari. Kadri iwezekanavyo kwenye kila somo, tumetoa maelezo kuhusu picha kutoka kwa picha za www.freebibleimages.org (FBI) ambazo zinaweza kupakuliwa bure kwenye tovuti yao. Viunga (links) maalum vya tovuti ya Free Bible Images kwa ajili

ya Masomo yote ya daraja zote na mfululizo wote wa Wakati na Biblia yanapatikana kwa barua pepe kutoka kwenye ofisi ya BES. Kama kuna kinakilishi (photocopier), baadhi ya picha za Bibletime zinaweza kufanywa kuwa kubwa, kupakwa rangi na kutumiwa kufundisha.

- **Rejelea Somo –** Tunashauri pale inapowezekana pawepo majaribio au vitendo ili kurahisisha ujifunzaji, na kama njia ya kufanya marudio ya habari.
- **Liishi Somo –** Sehemu hii imebeba kichwa cha habari, ‘kwa namna gani somo hili linatupa changamoto’ na pia mapendekezo kadhaa ya kazi inayoweza kufanywa kwa vikundi na majibu ya mtu binafsi kwa changamoto ya somo.

## Kufundisha Mstari Muhimu

1) Mstari unafaa kuandikwa kwenye karatasi au ubaoni na baadhi ya maneno kuondolewa huku watoto wakirudia ule mstari hadi pale maneno yote yatakapoondolewa na watoto kuurudia mstari bila kuangalia maneno.
2) Ili kuwaanzishia watoto Mstari muhimu, mwalimu anaweza kutumia:
    a) Njia ya Hangman yenye vikundi viwili (2 teams) – Unaweza kuwapa watoto baadhi ya nafasi za herufi za ule Mstari muhimu bila herufi zenyewe – Watoto watachagua herufi wanazozitaka mpaka mtu atakapoweza kuuona Mstari muhimu.
    b) Njia ya Sword Drill – watoto wanakuwa na Biblia na wote wanashindana kutafuta mstari huo wa Biblia na atakayeupata wa kwanza ataruhusiwa kuusoma kwa sauti.

## Kupangilia Muda

- **Ratiba –** Tumeweka ratiba sawa kwenye mwongozo wa kufundisha kila somo lakini mwalimu anaruhusiwa kubadilisha ratiba hii mara kwa mara kulingana na mahitaji ya darasa lake/ watoto anaowafundisha.
    1. Utangulizi na kuwaambia watoto habari husika – Takriban dakika 15
    2. Kufundisha Mstari muhimu – dakika 5 hadi10
    3. Kujaza nakala ya somo – dakika 20
    4. Maswali na shughuli zinginezo- dakika 5 hadi10

Kumbuka msemo muhimu:

“Niambie na nitasahau,
Nioneshe na nitakumbuka,
Nihusishe na nitaelewa”

## Mtaala wa Wakati na Biblia

| | Daraja 0<br>(Chekechea/Chini ya miaka mitano)<br>Daraja la Kwanza<br>(Miaka mitano hadi saba)<br>Daraja la Pili<br>(Miaka nane hadi kumi) | Daraja la Tatu<br>(Miaka kumi na mmoja hadi kumi na mitatu) | Daraja la Nne<br>(Miaka kumi na minne na zaidi) |
|---|---|---|---|
| SOMO LA KUANZIA | Somo la kuanzia – Utangulizi | Somo la kuanzia – Utangulizi | Somo la kuanzia – Utangulizi |
| MFULULIZO WA A | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Ibrahimu<br>6. Ibrahimu<br>7. Petro<br>8. Petro<br>9. Yakobo<br>10. Wakristo wa Kwanza<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maombi<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo na Kuanguka<br>2. Matukio ya Kwanza-Mwanzo<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maisha ya Ukristo<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi |
| MFULULIZO WA B | 1. Maisha ya kwanza ya Kristo<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Mifano<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Walioandika vitabu vya Injili<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yakobo na familia yake<br>7. Yusufu<br>8. Matendo ya Mitume 2: 42 – Njia iliyoko mbele<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Amri<br>12. Habari ya Krismasi |
| MFULULIZO WA C | 1. Danieli<br>2. Miujiza zaidi<br>3. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu na Samweli<br>6. Daudi<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Yona<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>3. Miujiza zaidi<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8 Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu ambao Mungu aliwatumia – Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Maneno ya Kristo<br>3. Nguvu za Bwana<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu zaidi wa Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi |

<table>
<tr><th></th><th>A7 – DARAJA LA 3<br>Somo la Kwanza – Maisha ya Yakobo<br>Mada – Mdanganyifu</th><th>A7 – DARAJA LA 4<br>Funzo la Kwanza – Maisha ya Yakobo<br>Mada – Mdanganyifu</th></tr>
<tr><td></td><td>Neno la Biblia: Mwanzo 25: 21-34 & 27: 1-29<br><br>Mstari Muhimu: Zaburi 32: 1<br><br>Tunajifunza kuwa:<br>1. Mungu anaweza kutusamehe tunapotenda dhambi.<br>2. Mungu anataka kubariki kila mmoja wetu.</td><td>Neno la Biblia: Mwanzo 25: 19-34 & 27: 1-41<br><br>Mstari Muhimu: Warumi 5: 8<br><br>Tunajifunza kuwa:<br>1. Kudanganya na kusema uwongo huleta shida na kutokuwa na furaha.<br>2. Mungu ana mpango kwa ajili ya maisha ya kila mmoja, hata maisha kama ya akina Yakobo.</td></tr>
<tr><td>TOA UTANGULIZI</td><td>Fafanua maana ya majaribu, na ni katika hali gani tunajaribiwa zaidi kusema uwongo. Orodhesha baadhi ya hali hizi na kufafanua kwa nini tunaweza kusema uwongo. Ongea pia juu ya kuwa na wivu na hali zinazosababisha kuwa na wivu, na kwa nini tunaweza kufanya hivyo.</td><td>Lazima tuishi na athari za matendo yetu. Husianisha hili na maisha yako mwenyewe, kwa mfano, ni lini wewe au mtu unayemjua alipata tatizo, labda hata na polisi kwa sababu ya kudanganya au kusema uwongo? Fikiria kwa nini kuvunja sheria (dhambi) kunapaswa kuadhibiwa.</td></tr>
<tr><td>KAMILISHA</td><td>Wasilisha Habari ya Biblia<br><br>Jadili na uelezee:<br>1. Baada ya Isaka kuomba, Rebeka akazaa mapacha, Esau alikuwa mkubwa na Yakobo mdogo wake.<br>2. Kulikuwa na upendeleo ndani ya nyumba; Isaka alimpenda Esau mwindaji na Rebeka alimpenda Yakobo ambaye alipenda kukaa nyumbani.<br>3. Elezea umuhimu wa haki za kuzaliwa katika nyakati za kale kule Mashariki ya Kati.<br>4. Esau alikuwa akiwinda na alikuwa na njaa; Yakobo alikuwa akipika kitoweo, lakini angempa kaka yake tu ikiwa atatoa haki yake ya mzaliwa wa kwanza.<br>5. Wakati Isaka alipokuwa mzee, alitaka kutoa baraka kwa mtoto wake mkubwa, lakini Rebeka na Yakobo walipanga njama kumdanganya Isaka ambaye alikuwa anakaribia kuwa kipofu. Esau alipokuwa akiwinda ili kumpatia baba yake chakula, Rebeka na Yakobo wakapika chakula haraka, Yakobo akajibadilisha na kumwambia Isaka kwamba yeye ni Esau, kwa hiyo akapokea baraka ya mzaliwa wa kwanza kutoka kwa baba yake.<br><br>Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.<br>Kamilisha Somo la Kwanza.<br>Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Esau sells his birthright to Jacob and Jacob deceives Esau (I)</td><td>Wasilisha Habari ya Biblia<br><br>Jadili na uelezee:<br>1. Baada ya Isaka kuomba, Rebeka akazaa mapacha, Esau alikuwa mkubwa na Yakobo mdogo wake.<br>2. Kulikuwa na upendeleo ndani ya nyumba; Isaka alimpenda Esau mwindaji na Rebeka alimpenda Yakobo ambaye alipendelea kukaa nyumbani.<br>3. Elezea umuhimu wa haki za kuzaliwa katika nyakati za kale kule Mashariki ya Kati.<br>4. Esau alikuwa akiwinda na alikuwa na njaa; Jacob alikuwa akipika kitoweo, lakini angempa kaka yake tu ikiwa atatoa haki yake ya mzaliwa wa kwanza.<br>5. Wakati Isaka alipokuwa mzee, alitaka kutoa baraka kwa mtoto wake mkubwa, lakini Rebeka na Yakobo walipanga njama kumdanganya Isaka ambaye alikuwa anakaribia kuwa kipofu. Wakati Esau akiwinda ili kumpatia baba yake chakula, Rebeka na Yakobo wakapika chakula haraka, Yakobo akajibadilisha na kumwambia Isaka kwamba yeye ni Esau, kwa hiyo akapokea baraka ya mzaliwa wa kwanza kutoka kwa baba yake.<br>6. Jadili mfano huu wa udanganyifu na uelezee umuhimu wa uaminifu.<br>7. Esau aliporudi akawa na hasira sana na akamsihi baba yake ampe baraka lakini nafasi hiyo haikuwepo tena. Alikuwa amepoteza haki yake ya mzaliwa wa kwanza na baraka zake.<br><br>Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.<br>Kamilisha Funzo la Kwanza.<br>Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Esau sells his birthright to Jacob and Jacob deceives Esau (I)</td></tr>
<tr><td>REJELEA SOMO</td><td>Fikiria juu ya dhambi ambazo Yakobo alifanya katika somo hili.<br>Je! Tunahitaji kusamehewa dhambi za aina gani? Fikiria kwa pamoja na kisha kwa faragha.<br>Tengeneza bodi ya grafiti, au mchoro wa buibui wa majibu mengi ya mwanafunzi.<br>Fikiria jinsi tunavyoweza kumwomba Mungu, na labda wengine kuomba msamaha. Soma Zaburi 32: 1-5 ili kukusaidia.</td><td>Fikiria jinsi ambavyo Esau alijisikia alipogundua udanganyifu na uwongo wa kaka yake na mama yake.<br><br>Fikiria nyakati ambazo ulipata tatizo kwa sababu ulisema uongo au kudanganya na uandike namna mbili ambazo utajaribu kuishi tofauti katika siku zijazo.</td></tr>
<tr><td>LIISHI SOMO</td><td>Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:<br>Andika dhambi kadhaa ambazo umetenda kwenye karatasi kisha ichane na kuitupa ndani ya ndoo ya takataka. Au andika baadhi ya dhambi kwenye mchanga au ardhi ya vumbi kisha futa muda mfupi baadaye.</td><td>Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:<br>1. Fikiria mipango ambayo Mungu alikuwa nayo kwa ajili ya Yakobo na ambayo anaweza kuwa nayo kwa ajili ya maisha yako kulingana na kanuni za Biblia kama Yeremia 29: 11.<br>2. Mualike Mungu akuonyeshe zaidi juu ya mustakabali wako. Kuwa na mtazamo chanya.</td></tr>
</table>

| | A7 – DARAJA LA 3<br>Somo la Pili – Maisha ya Yakobo<br>Mada – Mwota ndoto | A7 – DARAJA LA 4<br>Funzo la Pili – Maisha ya Yakobo<br>Mada – Mwota ndoto |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 27: 41-46 & 28: 10-22***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 28: 16***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ingawa Yakobo alikuwa amekosea, bado Mungu alikuwa pamoja naye na alimpenda sana.<br>2. Ndivyo ilivyo hata kwetu. | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 27: 41-46 & 28: 1-22***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 28: 16***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ingawa Yakobo alikosea, alikutana na Mungu kwa namna za kipekee ambapo alipewa ahadi kwa ajili ya maisha yake.<br>2. Siku zote Mungu hututendea kama vile alivyomtendea Yakobo. |
| TOA UTANGULIZI | Fikiria jinsi Mungu anavyotawala maisha yetu katika chochote tunachokifanya! Fikiria juu ya njia ambazo tunaweza kuwasiliana na watu wengine, na uzingatie kwamba wakati mwingine Mungu huzungumza nasi kwa njia mbalimbali. Waulize wanafunzi wafikirie juu ya njia ambazo Mungu anaweza kusema nasi leo. | Waulize wanafunzi kutoa mfano wa wakati ambapo mtu ambaye alikuwa na imani kwa Mungu alipata jambo ambalo siyo la kawaidi na la ajabu / jambo la kushangaza.<br>Je! Tunalazimika kuwa wakamilifu ili kupata mambo kama haya? |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Esau anawaza kumuua Yakobo baada ya kifo cha Baba yake. Rebeka anapendekeza kwamba Yakobo aende na kukaa na mjomba wake Labani hadi hasira ya Esau itakapokoma.<br>2. Isaka anambariki Yakobo na anapanga kwenda Padan Aramu.<br>3. Yakobo anapumzika usiku na kupata ndoto. Anaona ngazi inayoelekea Mbinguni. Kisha Bwana alizungumza naye, akimuahidi kuhusu nchi ambayo familia yake itairithi na pia kwamba atakuwa pamoja naye katika safari yake.<br>4. Yakobo anaamka na kuita mahali pale, Betheli, ikiwa na maana ya Nyumba ya Mungu.<br>5. Yakobo anaweka nadhiri kwa Mungu. Ikiwa Mungu atamtunza basi Yakobo atamfanya Bwana kuwa Mungu wake!<br>6. Fikiria masomo ambayo tunaweza kujifunza kutokana na muda wa Yakobo pale Betheli.<br>7. Fafanua na ueleze wazo la upendo wa Mungu kwa Yakobo lakini sio dhambi yake.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – God speaks to Jacob in a dream (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**i<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Esau anawaza kumuua Yakobo baada ya kifo cha Baba yake. Rebeka anapendekeza kwamba Yakobo aende na kukaa na mjomba wake Labani hadi hasira ya Esau itakapokoma.<br>2. Isaka anambariki Yakobo na anapanga kwenda Padan Aramu.<br>3. Yakobo anapumzika usiku na kupata ndoto. Anaona ngazi inayoelekea Mbinguni. Kisha Bwana alizungumza naye, akimuahidi kuhusu nchi ambayo familia yake itairithi na pia kwamba atakuwa pamoja naye katika safari yake.<br>4. Yakobo anaamka na kuita mahali pale, Betheli, ikiwa na maana ya Nyumba ya Mungu.<br>5. Yakobo anaweka nadhiri kwa Mungu. Ikiwa Mungu atamtunza basi Yakobo atamfanya Bwana kuwa Mungu wake!<br>6. Jadili na ueleze wazo la upendo wa Mungu kwa Yakobo lakini sio dhambi yake.<br>7. Jadili na ueleze mambo ya kushangaza ambayo tunaweza kuipata Mungu anapofanya kazi katika maisha yetu.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – God speaks to Jacob in a dream (I)** |
| REJELEA SOMO | Fanya kazi katika vikundi vidogo, ukitaja sehemu ambazo ulikuwa na ukatambua kuwa Mungu alikuwa na wewe, ukitumia kichwa "Mungu alikuwa na mimi hapa." Tafakari juu ya umuhimu wa ***Waebrania 13: 5*** katika maisha ya kila siku? | Je! Mungu amewahi kukupa ndoto? Je! Umewahi kuwa na ndoto yenye maana ya kiroho? Unafikiri ilikuwa na maana gani? Imekusaidiaje katika maisha?<br>Tafakari kwa namna gani nyingine Mungu anaweza kusema na watu leo. Anatoa ahadi gani ambazo zinaweza kuwafaa wanafunzi katika maisha yao ya kila siku? |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je! Kuna wakati ambapo ulitenda dhambi na bado ukatambua kwamba Mungu hajakukataa, na badala yake alikuwa akikubariki?<br>2. Je! Hali hii inakufanya uhisi vipi?<br>3. Unatarajia Mungu azungumze nawe vipi? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Tafiti kuhusu ndoto za kiroho na uwe tayari ili Mungu aweze kuongea na wewe kwa namna hii.<br>2. Tafuta katika Biblia ahadi nne za Mungu. Omba ukizitumia. |

| | A7 – DARAJA LA 3<br>Somo la Tatu – Maisha ya Yakobo<br>Mada – Kukatishwa tamaa | A7 – DARAJA LA 4<br>Funzo la Tatu – Maisha ya Yakobo<br>Mada – Kukatishwa tamaa |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 29: 1-30***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Wagalatia 6: 7***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Maisha ni kama kupanda na kuvuna.<br>2. Hakuna ahadi kwamba maisha yatakuwa rahisi kila wakati. | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 29: 1-30 & 31: 1-21***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Wagalatia 6: 7***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Maisha ni kama kupanda na kuvuna.<br>2. Anachosema Mungu, anamaanisha.<br>3. Tunapaswa kuwatendea wengine kama tunavyopenda kutendewa. |
| TOA UTANGULIZI | Zungumza juu ya kupanda na kuvuna katika bustani, mashamba, nk. na elezea kwamba mbegu yoyote inayopandwa itatoa mazao yale yale. Zungumza juu ya jinsi mwenendo wetu, mzuri au mbaya, unavyokuwa na matokeo mazuri au mabaya. Tunavuna kile tunachokipanda!<br>Fikiria kuhusu baadhi ya watu wa sasa ambao walikuwa na mwenendo mbaya na wakavuna matokeo mabaya. | Zungumza juu ya kupanda na kuvuna katika bustani, mashamba, nk. na elezea kwamba mbegu yoyote inayopandwa itatoa mazao yale yale. Zungumza juu ya jinsi mwenendo wetu, mzuri au mbaya, unavyokuwa na matokeo mazuri au mabaya.<br>Angalia kwenye magazeti ya hapa au majarida ya udaku kwa ajili ya mifano ya kupanda na kuvuna na tengeneza kolagi kwa kukata picha zao na kuongeza maneno. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Yakobo anafika Aramu na kukutana na wachungaji ambao wanawapa maji kondoo wao.<br>2. Raheli, binamu yake anakuja kuwanywesha maji kondoo wake na Yakobo anamsaidia, na anapomwambia baba yake Labani kwamba Yakobo amekuja, Labani anamkaribisha nyumbani kwao.<br>3. Yakobo anafanya kazi kwa Labani na anaahidiwa kwamba ikiwa atafanya kazi kwa Labani kwa miaka 7 anaweza kumuoa Raheli, ambaye amempenda sana.<br>4. Baada ya harusi, Yakobo aligundua kwamba alikuwa amedanganywa na alikuwa ameozeshwa Lea, dada yake Raheli.<br>5. Baadaye alipewa pia Raheli kuwa mke wake na ilibidi afanye kazi miaka mingine 7 kwa ajili ya Raheli.<br>6. *Fafanua jinsi ambavyo Yakobo, yule mwenye hila, alikuwa akivuna matokeo ya udanganyifu wake alioufanya miaka ya zamani kule nyumbani kwao.*<br>7. *Fafanua pia njia nyingi ambazo watu wanazitumia ili kukabiliana na kuvunjwa mioyo/ kukatishwa tamaa.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Jacob is deceived at his wedding (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Yakobo anafika Aramu na kukutana na wachungaji ambao wanawapa maji kondoo wao.<br>2. Raheli, binamu yake anakuja kuwanywesha maji kondoo wake na Yakobo anamsaidia, na anapomwambia baba yake Labani kwamba Yakobo amekuja, Labani anamkaribisha nyumbani kwao.<br>3. Yakobo anafanya kazi kwa Labani na anaahidiwa kwamba ikiwa atafanya kazi kwa Labani kwa miaka 7 anaweza kumuoa Raheli, ambaye amempenda sana.<br>4. Baada ya harusi, Yakobo aligundua kwamba alikuwa amedanganywa na alikuwa ameozeshwa Lea, dada yake Raheli.<br>5. Baadaye alipewa pia Raheli kuwa mke wake na ilibidi afanye kazi miaka mingine 7 kwa ajili ya Raheli.<br>6. *Fafanua jinsi ambavyo Yakobo, yule mwenye hila, alikuwa akivuna matokeo ya udanganyifu wake alioufanya miaka ya zamani kule nyumbani kwao.*<br>7. Baadaye Mungu anamwambia Yakobo arudi katika nchi yake alikozaliwa. Mungu amembariki na sasa ana makundi makubwa ya mifugo na familia kubwa. Hamuambii Labani kuwa anaondoka zake lakini anakimbia wakati ambao Labani yupo mbali na nyumbani kwake.<br>8. Fikiria juu ya mapungufu ya Yakobo na ufafanue jinsi ambavyo Mungu bado anafanya kazi katika maisha ambayo sio kamili.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Jacob is deceived at his wedding (I)** |
| REJELEA SOMO | Chagua mojawapo ya mifano kutoka Na.7 hapo juu na uuandike kwenye bango kubwa hapo darasani ili kila mmoja aweze kuona ya kwake. (Ikiwa stika zinapatikana, zinaweza kutumika kwa kubandikwa kwenye karatasi badala yake) | Fikiria mifano ya kupanda na kuvuna katika maisha ya watu, kwanza kwa njia mbaya, kisha kwa njia nzuri. Andika au chora kielelezo cha majibu yako ukijaribu kutoa majibu mawili kwa kila kikundi. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je, ni lini mara yako ya mwisho kuvunjika moyo/ kukatishwa tamaa?<br>2. Ni kwa namna gani hasa ulikabiliana na hali hiyo?<br>3. Je! Kuna njia bora zaidi ambayo ungeweza kuitumia kukabiliana na hali hiyo?<br>4. Je! Unaweza kuorodhesha mifano mitatu ya kupanda na kuvuna chini ya safu mbili/ columns kwa Lugha ya Kiingereza? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je! Unamjua mdanganyifu ambaye baadaye alidanganywa?<br>2. 2. Je! Unaweza kufikiria mifano mingine ya wakati ambapo waliotenda mabaya baadaye walipata mabaya hayo? |

| | A7 – DARAJA LA 3<br>Somo la Nne – Maisha ya Yakobo<br>Mada – Ugunduzi | A7 – DARAJA LA 4<br>Funzo la Nne – Maisha ya Yakobo<br>Mada – Ugunduzi |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 32 : 1-21 & 33: 1-11***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Yohana 1: 9***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Kwa msaada wa Mungu inawezekana kusamehe watu, hata kwa mambo mabaya ambayo walitutendea, kama ilivyotokea katika maisha ya Yakobo.<br>2. Mungu hutusamehe kila tunapotubu na kumuomba msamaha. | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 32: 1-32 & 33: 1-17***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Yohana 1: 9***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yakobo amepata shida maishani mwake lakini ilikuwa ni muhimu zaidi kwa Yakobo kukutana na Mungu kuliko kukutana na kaka yake aliyekuwa hajamwona kwa muda mrefu.<br>2. Ingawa ni mtu mzima sasa, Mungu bado alikuwa na mipango mipya kwa ajili ya maisha ya yakobo. |
| **TOA UTANGULIZI** | Wakumbushe wanafunzi kuwa Yakobo anamtii Mungu na kurudi nyumbani kwake, lakini ana hofu ya kukutana na Esau ambaye miaka ya zamani alikuwa ametishia kumuua. Fikiria kama Esau angekuwa tayari kumsamehe. Orodhesha mambo ambayo kwa kawaida yanakupata wewe: a) unapokosa kusamehe na b) unaposamehe. | Zungumzia kile kinachohitajika katika kukutana na mtu maalum, na jinsi tunavyoweza kujiandaa kwa ajili hiyo. Baada ya miaka ya kutokuwa na mawasiliano na Mungu, sasa Yakobo anakutana na Mungu. Yakobo hakubaki kama alivyokuwa tena, na akapokea msaada wa kwenda kuonana na Esau.<br>Ikiwezekana, fanya utafiti kwenye mtandao upate kitabu cha "The End of the Spear", au tazama kwenye DVD jinsi mke wa Jim Elliott alivyowasamehe waliomuua mumewe. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Fikiria sababu za Yakobo kuogopa kurudi nyumbani baada ya miaka mingi.<br>2. Yakobo anaogopa zaidi anapopata habari kwamba Esau anakuja kukutana naye na wanaume 400.<br>3. Yakobo anafanya vitu vitatu: 1) Anaigawanya familia yake katika makundi mawili akitumaini kuwa angalau kundi moja litakuwa salama ***(32: 7-8)***, 2) Anaomba ***(32: 9-12)***, 3) Anatuma zawadi kwa Esau. ***(32: 13-16)***<br>4. Usiku ule Yakobo anakuwa na wakati wa ajabu sana wa kukutana na Mungu na kutafuta baraka zake. ***(32: 22-31)***<br>5. Hofu ya Yakobo haikuwa na msingi. Esau anamkumbatia na anaonekana kwamba amemsamehe. Yakobo anaitambulisha familia yake na anamshawishi Esau apokee zawadi zake.<br>6. Bado hakurudi kwa baba yake na anamdanganya Esau tena kwa kutofika nyumbani mara moja.<br>7. *Fikiria ni kwa nini Yakobo alikuwa na mashaka na hakukubali ahadi za Mungu.*<br>8. *Toa mifano ya hofu na ueleze kwamba katika uhalisia hofu nyingi hazipo/ hazitokei, ingawa tunatumia muda mwingi kuziwaza.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Jacob returns to Canaan, and Jacob and Esau are re-united (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Fikiria sababu za Yakobo kuogopa kurudi nyumbani baada ya miaka mingi.<br>2. Yakobo anaogopa zaidi anapopata habari kwamba Esau anakuja kukutana naye na wanaume 400.<br>3. Yakobo anafanya vitu vitatu: 1) Anaigawanya familia yake katika makundi mawili akitumaini kuwa angalau kundi moja litakuwa salama ***(32: 7-8)***, 2) Anaomba ***(32: 9-12)***, 3) Anatuma zawadi kwa Esau. ***(32: 13-16)***<br>4. Usiku ule Yakobo anakuwa na wakati wa ajabu sana wa kukutana na Mungu na kutafuta baraka zake ***(32: 22-31)***<br>5. Hofu ya Yakobo haikuwa na msingi. Esau anamkumbatia na anaonekana kwamba amemsamehe. Yakobo anaitambulisha familia yake na anamshawishi Esau apokee zawadi zake.<br>6. Bado hakurudi kwa baba yake na anamdanganya Esau tena kwa kutofika nyumbani mara moja.<br>7. *Fikiria ni kwa nini Yakobo alikuwa na mashaka na hakukubali ahadi za Mungu.*<br>8. *Fikiria kuhusu habari za maisha halisi ya watu waliosamehe wengine.*<br>9. *Fikiria kuhusu madhara tunayojiletea sisi wenyewe na pia kwa wengine tunaposhindwa kusamehe.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Jacob returns to Canaan, and Jacob and Esau are re-united (I)** |
| **REJELEA SOMO** | Ukirejelea sehemu ya hapo juu, tumia baadhi ya mawazo yako kumwandikia Mungu barua. Waambie wanafunzi kufikiri kuhusu mambo ambayo wataungama kwa Mungu, mambo ambayo wataombea, na pia mambo ya kuwafanya kutoa shukurani. | Tafakari maana ya kukutana na Mungu<br>a) Je, ni wakati gani jambo hilo linaweza kufanyika?<br>b) Je, jambo hilo linawezaje kufanyika?<br>c) Je, ni kwanini linaweza kufanyika?<br>Waulize wanafunzi ikiwa wamewahi kukutana na Mungu kibinafsi. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kuna kitu gani cha kujifunza kutokana na kifungu hiki cha Biblia ambacho kinaweza kuhusiana na maisha yetu?<br>2. Toa mifano ya mtu aliyesamehewa hivi karibuni.<br>3. Je! Tunaweza kuomba msaada wa Mungu ili kumsamehe mtu? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Waulize wanafunzi ikiwa kuna mtu ambaye alishindwa kuwasamehe hivi karibuni, au amewasamehe.<br>2. Je, jambo hili liliwafanya wajihisi vipi?<br>3. Je! Kuna mtu ambaye wanapaswa kumsamehe? |

| | A8 – DARAJA LA 3<br>Somo la Kwanza – Kuwa Mkristo<br>Mada – Maombi ni nini? | A8 – DARAJA LA 4<br>Funzo la Kwanza – Kuwa Mkristo<br>Mada – Kujifunza kuhusu Maombi |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Zaburi 5: 1-8***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Zaburi 5: 2***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Maombi ni jambo la kipekee kwa sababu Mungu ni wa pekee.<br>2. Maombi ni kuzungumza na kumsikiliza Mungu.<br>3. Wakati mwingine maombi yetu hayajibiwi na kuna sababu za hali hiyo. | **Neno la Biblia:** ***Luka 11: 1-10 & Mathayo 6: 5-15***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 11: 9***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Tunapaswa kutambua kwamba maombi ni fursa ya kipekee sana.<br>2. Tunapaswa kusali mara nyingi.<br>3. Hatupaswi kujali zaidi kuhusu mambo yetu tunapofanya maombi binafsi. |
| **TOA UTANGULIZI** | Fikiria kuhusu matatizo/changamoto za kujaribu kuwasiliana na marafiki na familia ambazo ziko mbali. Fikiria ni ajabu kwamba tunaweza kuwasiliana na Mungu. Waulize wanafunzi kama huwa wanaomba. Kwa nini wanaomba? /Kwa nini hawaombi? | Fikiria kuhusu matatizo/changamoto za kujaribu kuwasiliana na marafiki na familia ambazo ziko mbali. Fikiria ni ajabu kwamba tunaweza kuwasiliana moja kwa moja na Mungu.<br>Fikiria kuhusu aina ya mambo ambayo tunapaswa kuyaombea.<br>Fikiria kama wanafunzi wamewahi kujibiwa maombi. Je! Walijihisi vipi maombi yao yalipojibiwa? |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Fikiria ni nani tunazungumza naye wakati tunapoomba na ufikiri kuhusu baadhi ya majina ambayo Daudi anayatumia katika Zaburi.<br>2. Fikiria kuhusu, je, ni wakati gani wa siku ambapo Daudi aliomba na kujadili ni wakati gani tunaweza kuomba.<br>3. Kutoka kwenye Zaburi fafanua kile kinachoweza kuzuia Mungu kusikia sala zetu.<br>4. Pia kutoka kwenye Zaburi, je, ni masomo gani tunaweza kujifunza ambayo yatatusaidia kujiandaa kuongea na Mungu katika maombi.<br>5. Daudi alikuwa na uhusiano wa kipekee na Bwana kwa sababu anataja Mfalme Wangu na Mungu Wangu katika mstari wa 2. Je, tunawezaje pia kuwa na uhusiano huo wa kipekee?<br>6. *Jadili na kueleza umuhimu wa maombi kwa mfano, maisha yangekuwaje bila maombi.*<br>7. Je, tunaweza kuombea nini?<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha: Hakuna vielelezo vya FBI vinavyofaa.** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Kipindi Fulani, Yesu alikuwa akisali na wanafunzi wake wakamuomba awafundishe jinsi ya kusali.<br>2. Fikiria ni nani tunazungumza naye tunaposali na fikiria kuhusu jina alilotumia Yesu.<br>3. Yesu alitoa mfano wa sala ulioanza na sifa kwa Mungu. Je! Ni sehemu gani ya sala zetu inapaswa kuwa na sifa?<br>4. Fikiria kuhusu mahitaji makuu MATATU ambayo Yesu aliyaombea katika ule mfano wake wa sala.<br>5. Soma mfano ambao Yesu aliwaambia ***(Luka 11: 5-10)*** na ufikirie juu ya somo kuu kuhusu kuomba bila kukoma katika mfano ambao Yesu alikuwa akifundisha.<br>6. Fikiria juu ya masomo ambayo Yesu alifundisha kuhusu maombi katika ***Mathayo 6: 5-15***.<br>7. *Fikiri ni kwa nini tunaomba zaidi wakati ambapo mambo hayaendi vizuri.*<br>8. *Pia fikiria kwa nini wakati mwingine tunapata ugumu wa kufanya maombi.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Parable of the midnight visitor (I)** |
| **REJELEA SOMO** | Je! Kuna vitu na watu wanaohitaji sala zetu? Tunapaswa kusali mara ngapi? Na kwa muda gani?<br>Fikiria juu ya maombi ya mtu mwingine katika Biblia na masomo ambayo tunaweza kujifunza kutokana na maisha yao ya maombi. | Kwa kifupi zungumza kuhusu vipengele VITANO kuhusu maombi kama vilivyotajwa kwenye Funzo la Kwanza na uwaombe wanafunzi wafanye kazi kwa vikundi kuandaa sala zenye vipengele hivyo vyote. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Je! Unapaswa kuzungumza zaidi au kusikiliza zaidi katika sala? Pengine tunapaswa kuanza kusikiliza kile ambacho Mungu anasema wakati ambao tunafanya maombi. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Fikiria juu ya hali za kibinafsi, katika familia, katika jamii ulipo, nchi na ulimwenguni kote ambazo zinaweza kuombewa. Fikiria kushukuru kwa sala ambazo zimejibiwa. |

| | A8 – DARAJA LA 3<br>Somo la Pili – Kuwa Mkristo<br>Mada – Je, Mungu anasikiliza sala zetu? | A8 – DARAJA LA 4<br>Funzo la Pili – Kuwa Mkristo<br>Mada – Kujifunza kuhusu Biblia |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Luka 18: 9 -14***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yakobo 4: 6***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Hatuhitaji kwenda Kanisani ili kumuomba Mungu: tunaweza kuomba mahali popote na wakati wowote.<br>2. Mungu anataka tuwe wanyenyekevu na waaminifu katika maombi. | **Neno la Biblia:** ***Matendo 17: 10-14 & 2 Timotheo 3: 14-17***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Zaburi 119: 105***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ni muhimu kusoma Biblia.<br>2. Tunaweza kuamini Biblia kwa sababu ni Neno la Mungu. |
| TOA UTANGULIZI | Rejelea mafunzo ambayo umejifunza juu ya maombi katika Somo la Kwanza. Biblia inasema "Kiburi hutokea kabla ya anguko." ***(Mithali 16: 18)***. Je, unafikiria hii inamaanisha nini. Elezea kutokana na hali halisi ya maisha au habari ya kutunga. | Kuna Biblia nyingi ulimwenguni kuliko kitabu kingine chochote. Kwa miaka mingi nchi zilijaribu kuipiga marufuku, kuichoma au hata kuizika lakini bado ipo leo. Hii ni kwa sababu ni Neno la Mungu. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Yesu alikuwa akifundisha kwamba tunapaswa kuomba bila kukoma na tusikate tamaa. ***(mstari wa 1)***<br>2. Alikuwa pia akielezea kwamba wale waliokuwa na kiburi na kukosa unyenyekevu hawakuwa katika mtazamo sahihi wa kuomba. ***(mstari wa 9)***<br>3. Angalia ni mara ngapi mtu wa kidini (Mfarisayo) alitumia neno "mimi".<br>4. Waombe wanafunzi waelezee sala na mtazamo wa mtoza ushuru.<br>5. *Tofautisha mitazamo tofauti ya sala ambazo watu hawa wawili walikuwa nayo.*<br>6. *Fikiria ni mtu yupi alimpendeza Mungu zaidi na kwa nini.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Parable of the Pharisee and the Tax collector (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Kwa Wakristo, Biblia ni kitabu muhimu zaidi, lakini tunawezaje kuwa na uhakika kuwa Biblia ni kweli?<br>2. Neno la Biblia linatuambia kwamba Maandiko yote yana pumzi ya Mungu, ikimaanisha yametoka kwa Mungu. Mungu hawezi kusema uwongo kwa hivyo tunatambua kwamba Biblia ni kweli.<br>3. Mambo mengi yalitabiriwa katika Agano la Kale na kweli yakatokea wakati fulani katika mamia ya miaka baadaye. Kwa mfano marejeleo yote katika Agano la Kale kuhusu kuzaliwa kwa Yesu.<br>4. Takriban watu 40 tofauti waliandika sehemu za Biblia katika kipindi cha karne nyingi, lakini kuna mada moja kuu na ujumbe mmoja unaoleta umoja katika Kitabu hicho.<br>5. Kusoma Biblia na kufuata mafunzo yake kunaweza kubadilisha maisha ya watu kwa msaada wa Roho Mtakatifu.<br>6. Ndiyo maana Biblia ni muhimu sana. Fikiria kuhusu sababu nyingi ambazo zinatufanya kusoma Biblia.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha: Hakuna vielelezo vinavyofaa vya FBI.** |
| REJELEA SOMO | Kwenye kipande cha karatasi andika sifa alizodhihirisha mtoza ushuru na kwenye kipande kingine, sifa ambazo Mfarisayo alizidhihirisha. | Fikiria juu ya Mstari Muhimu na kisha chora picha ya mihimili ya mwanga (beams of light kwa Kiingereza) kutoka angani. Chini yake chora au andika baadhi ya mambo unayohitaji yafikiwe na nuru ya Mungu kwa mfano, uamuzi ambao unataka kufanya, msaada wakati unapojisikia kuvunjika moyo/ kukasirika. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je! Neno "unyenyekevu" linamaanisha nini na tunawezaje kuwa wanyenyekevu zaidi? Toa mifano ya jinsi tunavyoweza kuonesha unyenyekevu.<br>2. Je! Neno "kiburi" linamaanisha nini na tunawezaje kuacha kiburi? Toa mifano ya jinsi tunavyoweza kuonesha kiburi. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Ni vitu gani vya kivitendo ambavyo vinaweza kurahisisha/ kutusaidia kwenye usomaji wa Biblia?<br>2. Fikiria kuhusu kumuomba Mungu atusaidie kusoma Biblia mara nyingi, kuielewa vizuri na kuitumia maishani mwetu. |

| | A8 – DARAJA LA 3<br>Somo la Tatu – Kuwa Mkristo<br>Mada – Je, tunapaswa kuomba vipi? | A8 – DARAJA LA 4<br>Funzo la Tatu – Kuwa Mkristo<br>Mada – Kuishi kwa ajili ya Mungu |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mathayo 6: 5-15***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 6: 8***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Tunapaswa kusali mara kwa mara na sio tu wakati ambao mambo hayaendi vizuri.<br>2. Hatuitaji maombi yetu kuwa ya dhana au ya muda mrefu.<br>3. "Sala ya Bwana" imekusudiwa kutusaidia kufanya au kupangilia sala zetu. | **Neno la Biblia:** ***Yohana 15: 1-17 & Wagalatia 5:22-23***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 15: 5***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Wakristo wanapaswa kuendelea zaidi na zaidi katika kufanana na Yesu.<br>2. Siri ni kukaa karibu naye kama ilivyoelezewa kwenye mzabibu na matawi yake.<br>3. Wakristo wanahitaji mguso wa Mungu katika kupogoa (kuondoa matawi yasiyozaa au pruning kwa Kiingereza) ili kuzaa matunda zaidi. |
| TOA UTANGULIZI | 1. Rejelea Masomo ya 1 & 2 na yote ambayo tayari wanafunzi wamejifunza kuhusu maombi. Fikiria ni kwanini watu wengi huona ni vigumu kuomba mara kwa mara.<br>2. Kuna faida zipi za kuomba kwa sauti kubwa ili kusaidia kuwa makini?<br>3. Kuna faida gani katika kuandika maombi ili kusaidia kuwa na maneno sahihi? | 1. Fikiria kuhusu Wakristo wenye matunda ambao hudhihirisha tunda la Roho na fikiria jinsi maisha yao yalivyo na mguso/matunda.<br>2. Elezea jinsi Mungu anavyoweza kufanya kazi katika maisha yetu kuondoa vitu visivyo na msaada na labda tabia za dhambi, kama vile mtunza bustani anavyopogoa mzabibu. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Bwana alifundisha juu ya maombi katika Mafunzo ya Mlimani.<br>2. Elezea kwa nini maombi ni ya faragha kati yetu na Mungu.<br>3. Elezea kwa nini kurudiarudia sala au kuifanya baada ya kuikariri sio sala ya kweli.<br>4. Jadili kwa nini maombi ni ya muhimu ikiwa "Baba anajua kile tunachohitaji kabla ya kumuomba".<br>5. Fikiria juu ya Mfano wa sala ya Bwana katika suala la Sifa na Mahitaji ya Maombi.<br>6. Fikiria kuhusu umuhimu wa kuamini kuwa Mungu atajibu tukiomba na kuweka sala zetu katika vitendo.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha: FBI- Hakuna vielelezo vinavyofaa vya FBI.** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Elezea picha ya Baba kama mtunza bustani, Bwana kama mzabibu na Wakristo kama matawi.<br>2. Elezea kwamba Mungu anataka kuona maisha yetu yakiwa na matunda, na hii inadhihirishwa vyema katika ***Wagalatia 5: 22-23.***<br>3. Fikiria kuhusu mwonekano wa miti ya matunda kabla na baada ya kupogolewa na kwa nini jambo hili ni muhimu katika kuongeza mavuno ya matunda.<br>4. Tofautisha kwenye ***Wagalatia 5: 19-20*** ambapo kuna tunda la tabia ya asili ya mwanadamu bila utendaji wa Roho Mtakatifu na bila imani katika Kristo.<br>5. Wakumbushe wanafunzi kwamba kusudi la Mungu ni kwamba kama Wakristo tunapaswa kuwa kama Kristo, ambaye alidhihirisha tunda lote la Roho katika maisha yake.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha: FBI- Hakuna vielelezo vinavyofaa vya FBI.** |
| REJELEA SOMO | Fikiria kuhusu ***1 Timotheo 2: 1*** na muwe na majadiliano ya aina mbali mbali za sala.<br>Fikiria kuhusu maeneo ambayo tunaweza kusali kibinafsi au kwa faragha. Yaorodheshe wanafunzi wanapoendelea kupendekeza maeneo hayo. | Eleza kwa muhtasari masomo muhimu uliyojifunza katika Funzo hili. Sisitiza kwamba jambo muhimu ni kukaa ndani Yake kama inavyoelezewa katika ***Yohana 15: 4-5.*** |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Maombi sio jambo la kufanyika kimyakimya bali ni jambo linalohusisha hisia. Je, jambo hili linaweza kuwa na maana gani kwako kwa wakati huu. Omba msaada wa Mungu ili kuwa na imani unaposali.<br>Tumia muundo/ mpangilio uliopewa katika Sala ya Bwana ili kuwasaidia wanafunzi kuandaa sala zao wenyewe. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Waelekeze wanafunzi wasome ***Wagalatia 5: 22-23*** wakiwa kwenye hali ya maombi. Kisha wamwombe Mungu awaoneshe ni sifa/tunda gani wanahitaji msaada wa Mungu ili kuwa nalo. |

<table>
<tr><th></th><th>A8 – DARAJA LA 3<br>Somo la 4 – Kuwa Mkristo<br>Mada – Je, Mungu anajibu maombi?</th><th>A8 – DARAJA LA 4<br>Funzo la 4 – Kuwa Mkristo<br>Mada – Kumtolea Mungu</th></tr>
<tr><td></td><td>Neno la Biblia: 1 Samweli 1: 1-20<br><br>Mstari Muhimu: 1 Samweli 1: 20<br><br>Tunajifunza kuwa:<br>1. Maombi yetu hayajibiwa wakati wote kama tunavyotaka, au haraka kama tunavyotamani iwe.<br>2. Majibu ya Mungu na mipango yake daima ni bora kuliko yetu.</td><td>Neno la Biblia: Marko 12: 41-44 & Mathayo 6: 1-4<br><br>Mstari Muhimu: 2 Wakorintho 9: 7<br><br>Tunajifunza kuwa:<br>1. Tunapaswa kumtolea Mungu kwa moyo mkunjufu, kama tabia muhimu katika maisha yetu ya Kikristo.<br>2. Kumtolea Mungu sio kwa kutoa hela tu.</td></tr>
<tr><td>TOA UTANGULIZI</td><td>Mtambulishe Hana na hali yake.<br>Andaa onyesho la ukutani kwa kutumia picha na maneno ili kuonesha hisia za Hana:<br>KABLA YA SALA + BAADA YA SALA.</td><td>Katika vikundi vidogo, kaa kwenye duara na uandike orodha ya mambo ambayo Mungu hutupatia, na kisha vitu ambavyo tunaweza kumpa Bwana.</td></tr>
<tr><td>KAMILISHA</td><td>Wasilisha Habari ya Biblia<br><br>Jadili na uelezee:<br>1. Eleza kwa ufupi hali ya Hana na familia yake. Pia elezea safari ya kila mwaka kwenye Nyumba ya Bwana kwa ajili ya dhabihu na ibada.<br>2. Eleza jinsi ambavyo Hana alijihisi alipokuwa hana watoto na alipokuwa akichokozwa na Penina.<br>3. Fikiria juu ya sala ya Hana na ahadi aliyompa Bwana.<br>4. Elezea hisia za yule kuhani Eli wakati ambapo Hana alikuwa akiomba.<br>5. Eleza jinsi Mungu alivyojibu maombi ya Hana.<br>6. Fikiria jinsi alivyojihisi kuwa na hali ya utofauti baada ya kusali na kumwachia Bwana haja yake.<br><br>Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.<br>Kamilisha Somo la Nne.<br>Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI- Samuel is born (I)</td><td>Wasilisha Habari ya Biblia<br><br>Jadili na uelezee:<br>1. Elezea hali ilivyokuwa pale Hekaluni wakati ambapo Yesu alikuwa akiwatazama watu wakitoa hela.<br>2. Eleza kwa nini sadaka ya mjane maskini ilikuwa tofauti sana na sadaka walizozitoa wengine.<br>3. Kwa nini Yesu alipendezwa sana na sadaka ndogo ya mwanamke huyo?<br>4. Tukio hili linatufundisha nini kuhusu kumpa Bwana muda wetu, talanta zetu na hazina zetu?<br>5. Kwa nini Mungu anatuagiza kumtolea kwa siri?<br>6. Fikiria juu ya ahadi ya Mungu kwa wale ambao humtolea kwa siri.<br><br>Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.<br>Kamilisha Funzo la Nne.<br>Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI- The widow who gave everything (I)</td></tr>
<tr><td>REJELEA SOMO</td><td>1. Waulize wanafunzi kama wamewahi kujisikia huzuni kwa ajili ya jambo fulani.<br>2. Je, wangefanya nini ili kupata msaada katika muda huo.<br>3. Jadili ikiwa kuna mtu amewahi kujisikia vizuri zaidi baada ya kumtwika Bwana fadhaa zake.</td><td>1. Fikiria ni njia zipi tunaweza kuzitumia katika kumtolea Bwana.<br>2. Chagua jambo moja ambalo linaweza kufanyiwa kazi kutokana na Funzo la leo.<br>3. Wape changamoto wanafunzi wahakikishe kuwa wana nia njema wanapomtolea Mungu.</td></tr>
<tr><td>LIISHI SOMO</td><td>Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:<br>Fikiria juu ya watu ambao wangefaidika kwa kujua kwamba Mungu anaweza kubeba fadhaa zao na kuwafanya wajisikie vizuri. Je! Watu hawa wanaweza kutembelewa hivi karibuni na kuambiwa habari hii?</td><td>Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:<br>Tafuta mistari mingine yoyote ya Biblia inayohusiana na utoaji kwa mfano "Yesu alisema 'ni heri kutoa kuliko kupokea'." (Matendo 20: 35.) Muombe Mungu akusaidie kuelewa kanuni hii.</td></tr>
</table>

| | A9 – DARAJA LA 3<br>Somo la Kwanza – Safari za Paulo<br>Mada – Mtesaji | A9 – DARAJA LA 4<br>Funzo la Kwanza – Mtume Paulo<br>Mada – Kubadilika Kwake |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Matendo 9: 1-19***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***2 Wakorintho 5: 17***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Paulo alibadilishwa baada ya kukutana na Kristo.<br>2. Bado Mungu anabadilisha maisha hata leo. | **Neno la Biblia:** ***Matendo 9: 1-30***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***2 Wakorintho 5: 17***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ni Mungu tu anayeweza kubadilisha maisha.<br>2. Kuwa Mkristo kunaweza kuwa na ugumu wake, lakini Mungu yuko pamoja na Wakristo hasa katika nyakati ngumu. |
| **TOA UTANGULIZI** | Mtambulishe Sauli kama mmoja wa wahusika wakuu katika Agano Jipya. Fafanua uhusiano wake na kifo cha Stefano. ***(Matendo 6: 58)***<br>Tumia mfano wa kiwavi anayebadilika kuwa kipepeo katika kutambulisha dhana ya uongofu/kubadilika. | Mtambulishe Sauli kama mmoja wa wahusika wakuu katika Agano Jipya. Fafanua uhusiano wake na kifo cha Stefano. ***(Matendo 6: 58)***<br>Tumia mfano wa kiwavi anayebadilika kuwa kipepeo katika kutambulisha dhana ya uongofu/kubadilika. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Fafanua kwamba Paulo anatajwa kama Sauli hadi baadaye sana katika habari.<br>2. Toa maelezo kuhusu safari yake ya kuelekea Dameski.<br>3. Fafanua kwa makini kilichotokea, na kile kilichosemwa wakati Sauli alipokutana na Bwana. Simulizi ambazo Paulo alizitoa baadaye zinaweza kusaidia. ***(Matendo 22: 1-13, na 26: 9-18)***<br>4. Eleza kile kilichotokea baada ya kupelekwa Dameski na changamoto aliyopewa.<br>5. Fikiria juu ya maana ya neno 'uongofu'. Uongofu ni kazi ya neema ya Mungu katika kuumba mtu mpya katika Kristo. Husianisha hili na kuzaliwa mara ya pili. (Yohana 3: 3).<br>6. Fafanua jinsi Paulo alivyobadilishwa baada ya kukutana na Kristo.<br>7. Sisitiza umuhimu wa ujumba huu katika imani ya Kikristo.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – The Conversion of Saul (Paul) (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Fafanua kwamba Paulo anatajwa kama Sauli hadi baadaye sana katika habari.<br>2. Toa maelezo kuhusu safari yake ya kuelekea Dameski.<br>3. Fafanua kwa makini kilichotokea, na kile kilichosemwa wakati Sauli alipokutana na Bwana. Simulizi ambazo Paulo alizitoa baadaye zinaweza kusaidia. ***(Matendo 22: 1-13, na 26: 9-18)***<br>4. Eleza kile kilichotokea baada ya kupelekwa Dameski na changamoto aliyopewa.<br>5. Kuwa Mkristo kamwe sio jambo rahisi. Eleza baadhi ya matatizo ambayo Sauli alikabiliana nayo katika siku zake za kwanza za kumfuata Bwana.<br>6. Fikiria kuhusu asili ya uongofu kama kazi ya neema ya Mungu katika kuumba mtu mpya katika Kristo. Husianisha hili na kuzaliwa mara ya pili ***(Yohana 3: 3).***<br>7. Pia zingatia jinsi ambavyo Sauli hakufanywa 'mtu wa kidini'; tayari alikuwa mtu wa kidini kabla ya uongofu wake.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – The Conversion of Saul (Paul) (I)** |
| **REJELEA SOMO** | Unda onyesho la ukutani lenye mada 'Sauli - kabla na baada'. | Chagua moja ya makusudi ya kujifunza na uandike sala kuelezea jinsi kusudi hilo linavyoweza kuathiri maisha yako. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Wape changamoto wanafunzi kuhusu hali yao wenyewe.<br>2. Tunaweza kujifunza nini kuhusu utii kutokana na mfano wa Anania? Tengeneza orodha ya 'kufanyia kazi' kulingana na kile ambacho wanafunzi wanaweza kujifunza kuhusu utii.<br>3. Fikiria njia ambazo Wakristo wanaweza kuwa faraja kwa Mkristo mpya. Ziorodheshe na kuandaa mpango wa utekelezaji. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Wape changamoto wanafunzi kuhusu hali yao wenyewe.<br>2. Waombee leo Wakristo ambao wanakabiliwa na mateso.<br>3. Soma ***1 Timotheo 1: 12-16***. Fikiria juu ya kuwashirikisha marafiki ambao hawajaokoka ***mstari wa 15.*** |

| | A9 – DARAJA LA 3<br>Somo la Pili – Safari za Paulo<br>Mada – Matatizo | A9 – DARAJA LA 4<br>Funzo la Pili – Mtume Paulo<br>Mada – Safari zake |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Matendo 9: 19-30***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Warumi 1: 16***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Wakati mwingine inaweza kuwa vigumu kuwa Mkristo kwani sio kila mtu anathamini ujumbe wa Injili.<br>2. Ni muhimu kuwatia moyo Wakristo wapya. | **Neno la Biblia:** ***Matendo 11: 19-26; 13: 1-12***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 13: 12***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Wokovu ni mwanzo wa maisha mapya katika Kristo.<br>2. Ni muhimu kuwafundisha Wakristo wapya ili waweze kukua katika uelewa wao kuhusu maisha ya Kikristo. |
| **TOA UTANGULIZI** | Fafanua umuhimu wa kutia moyo. Waombe wanafunzi watoe mifano kuhusu wakati gani walitiwa moyo katika maisha yao na uwaeleze ni kwanini hili lilikuwa jambo muhimu sana. | Kwa kutumia mifano, fafanua jinsi gani chakula ni muhimu kwa ukuaji wetu wa mwili. Anza kuzungumzia wazo la ukuaji wa kiroho kwa Wakristo. Kama Biblia zinapatikana muombe mmojawapo asome ***1 Petro 2: 2 na 2 Petro 3: 18***. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Elezea kile kilichotokea wakati Sauli alipoanza kuhubiri huko Dameski, na pia eleza ujumbe wake ulikuwa upi.<br>2. Eleza kwanini Wayahudi walimchukia na pia jinsi alivyofanikiwa kutoroka.<br>3. Fafanua asili ya matatizo ya Sauli na kwa nini watu walipinga ujumbe wa Injili. Kwa nini Sauli hakuionea haya Injili? (angalia Mstari Muhimu)<br>4. Elezea matatizo aliyokabiliana nayo aliporudi Yerusalemu.<br>5. Zungumza jinsi Barnaba alivyokuwa wa muhimu kwa Sauli na umuhimu wa kutiana moyo katika maisha ya Kikristo. Soma ***1 Samweli 30: 6.***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – The conversion of Paul (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Baada ya kifo cha Stefano, Wakristo walitawanyika katika eneo kubwa na wengine wakafika Antiokia.<br>2. Walieneza habari njema kuhusu Yesu na wengi wakaamini na kumgeukia Bwana.<br>3. Barnaba alitumwa kutoka Yerusalemu kusaidia Wakristo wapya. Alitambua kuwa ilikuwa ni kazi kubwa kwa hiyo akamchukua Sauli hadi Antiokia na kwa mwaka mzima wakafundisha watu wengi katika Kanisa.<br>4. Katika kipindi hicho Roho Mtakatifu akaliambia Kanisa liwatume Barnaba na Sauli kwenda kufanya kazi mpya.<br>5. Wakaenda Kipro ambapo walipata upinzani wa mtu anayeitwa Elima, aina ya mchawi ambaye alijaribu kumzuia mmoja wa wanaume viongozi, Sergio Paulo, asiwe Mkristo. Sauli akamkemea, Elima akapofushwa na Sergo Paulo akamwamini Bwana Yesu.<br>6. Sisitiza umuhimu wa kuhubiri Neno katika uinjilisti. ***(Matendo 11: 19-20).***<br>7. Sisitiza pia umuhimu wa kukua kama Wakristo. ***(1 Petro 2: 2).***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Paul and Barnabas visit Cyprus (I)** |
| **REJELEA SOMO** | Jadili baadhi ya magumu ya maisha ya Kikristo mkimtumia Sauli kama mfano. | Rejelea somo ukitumia maswali yafuatayo:<br>1. Je, utume wa Paulo na Barnaba ulifanikiwa? Elezea jibu lako.<br>2. Masomo gani tunajifunza kutokana na Paulo alivyokabiliana na Elima kuhusiana na nguvu ya Mungu dhidi ya roho wabaya? |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Wakati mwingine watu wanatarajia maisha yawe 'hayana matatizo' wakati wanapokuwa Wakristo. Unafikiria Paulo angewapa ushauri gani watu wenye mtazamo huu? Zingatia ***2 Wakorintho 11: 23-33.***<br>2. Andika sala ya kutia moyo kwa Wakristo wanaokabiliwa na ugumu. Buni alamisho (bookmark) yenye sala juu yake na umpatie Mkristo unayemjua ambaye inawezekana kuwa anakabiliwa na ugumu. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Waelekeze wanafunzi wazungumze na Mhubiri Mkristo unayemjua na kumuliza juu ya shuhuda za kipekee za wokovu au madadiliko ambayo amewahi kupata katika huduma yake. Je! Jambo hili linakupa changamoto ipi?<br>2. Jadiliana na kiongozi wa Kikristo unayemjua kuhusu jinsi ya kukuza uelewa mzuri wa Biblia na kubuni mpango wako mwenyewe wa kusoma Biblia. |

| | A9 – DARAJA LA 3<br>Somo la Tatu – Safari za Paulo<br>Mada – Mhubiri | A9 – DARAJA LA 4<br>Funzo la Tatu – Mtume Paulo<br>Mada – Kuhubiri Kwake |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Matendo 13: 1-12***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 13: 12***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Roho Mtakatifu alikuwa akitenda kazi na ujumbe wa Injili ulikuwa ukitangazwa katika maeneo mapya.<br>2. Kunaweza kuwepo upinzani wa kishetani dhidi ya Injili. | **Neno la Biblia:** ***Matendo 13: 13-52***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 13: 49***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ujumbe kuhusu Kristo una msingi wake katika Agano la Kale na kwamba kifo na kufufuka kwa Kristo kulikuwa ndani ya mpango wa Mungu.<br>2. Msamaha wa dhambi ni kupitia Kristo tu. |
| TOA UTANGULIZI | Wape wanafunzi utangulizi wa faraka/ mapambano kati ya Mungu na Shetani. Fuatilia hili kuanzia kwenye Bustani ya Edeni na ufafanue habari ya Anguko. Eleza kwamba Shetani bado yuko hai kwa namna tofauti tofauti na anapinga mahubiri ya Injili ya Bwana Yesu. | Waambie wanafunzi wafikirie kuhusu umuhimu wa msamaha. Wafikirie hali za kila siku ambapo wanaweza kumsamehe mtu. Tafakari ni kwanini tunahitaji msamaha wa Mungu. Fafanua jinsi ambavyo Kristo ni wamuhimu katika ujumbe wa Kikristo wa msamaha wa dhambi. Chunguza mitazamo kadhaa potofu kuhusu msamaha. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Baada ya kifo cha Stefano, Wakristo walitawanyika katika eneo kubwa na wengine wakafika Antiokia.<br>2. Walieneza habari njema kuhusu Yesu na wengi waliamini na kumgeukia Bwana.<br>3. Barnaba alitumwa kutoka Yerusalemu ili kuwasaidia Wakristo wapya. Alitambua kuwa hii kazi ilikuwa kubwa kwa hiyo akamchukua Sauli hadi Antiokia na kwa mwaka mzima wakafundisha watu wengi katika Kanisa.<br>4. Katika kipindi hicho Roho Mtakatifu akaliambia Kanisa liwatume Barnaba na Sauli kwenda kufanya kazi mpya.<br>5. Wakaenda Kipro ambapo walipata upinzani wa mtu anayeitwa Elima, aina ya mchawi ambaye alijaribu kumzuia mmoja wa wanaume viongozi, Sergio Paulo, asiwe Mkristo.<br>6. Sauli akamkemea, Elima akapofushwa na Sergo Paulo akamwamini Bwana Yesu.<br>7. *Fafanua uhalisia na asili ya kumilikiwa na pepo.*<br>8. *Fafanua umuhimu wa ujumbe wa Injili katika siku hizo na leo.*<br>9. *Tafakari ni kwanini hukumu ya Mungu ilimuangukia Elima.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Paul and Barnabas visit Cyprus (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Sasa Paulo anawasili Antiokia nyingine. (Pisidia)<br>2. Katika ujumbe wake wa kwanza, aliwapa maelezo ya kina kuhusu historia ya Wayahudi, akimalizia na kuja kwa Yesu, kifo Chake, na ufufuo. Alihitimisha kwa kusema kwamba "kupitia kwa Yesu msamaha wa dhambi unahubiriwa kwenu." ***(mstari wa 38)***<br>3. Baada ya ujumbe wake wa kwanza katika sinagogi, Paulo alialikwa kurudi kwenye Sabato iliyofuata.<br>4. Sabato iliyofuata takriban mji wote ulihudhuria kumsikia Paulo jambo ambalo liliwafanya viongozi wa Kiyahudi waone wivu sana.<br>5. Paulo alisema kwamba kwa vile walikuwa wamekataa Neno la Mungu, sasa atawaendea Mataifa kama ***Isaya 49: 6*** inavyosema.<br>6. *Elezea kwanini viongozi wa Kiyahudi walitaka Kristo afe.*<br>7. *Zingatia ni kwanini Yesu alilazimika kufa na jinsi kifo na ufufuo wa Kristo vilivyokuwa sehemu ya mpango wa Mungu.*<br>8. *Fikiria kuhusu ule upekee wa Kristo kama Mwokozi.* ***(tazama mstari wa 38-39)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Paul and Barnabas in Antioch and Iconium (I)** |
| REJELEA SOMO | Rejelea mafunzo kwa kuuliza wanafunzi waelezee jinsi Mungu anavyomshinda Shetani katika somo ambalo tumejifunza hivi karibuni. | Wape wanafunzi jaribio kutokana na mafunzo ya leo kama njia ya kurejelea somo. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Tofautisha mwitikio wa Elima na Sergio Paulo na ujumbe wa Injili. Wape wanafunzi changamoto kutokana na majibu yao kuhusu Injili.<br>2. Katika filamu nyingi leo, mada ya uchawi ni ya kawaida mf.Filamu za Bongo Movies, Afro cinema n.k . Je! Wakristo wanapaswa kutazama sinema hizi? Fanyeni majadiliano darasani. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je! Upekee wa Kristo kama Mwokozi unaleta changamoto gani kwenye utamaduni wetu?<br>2. Soma ***Waefeso 4: 32*** na uwape wanafunzi changamoto ya jinsi gani maneno ya Paulo kuhusu msamaha yanavyowaathiri! |

| | **A9 – DARAJA LA 3**<br>**Somo la Nne – Safari za Paulo**<br>**Mada – ‘Mji Uliogawanyika’** | **A9 – DARAJA LA 4**<br>**Funzo la Nne – Mtume Paulo**<br>**Mada – Matatizo Yake** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Matendo 13: 13-16; 42-52***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 13: 49***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ni muhimu kusikiliza Neno la Mungu.<br>2. Ujumbe kuhusu Kristo ni kwa ajili ya kila mtu na ulileta furaha kwa wale walioupokea. | **Neno la Biblia:** ***Matendo 14: 1-28***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Marko 16: 20***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ujumbe wa Kristo unawagawa watu na kwamba upinzani wa ujumbe wa Kikristo unaweza kuwa mkubwa mno.<br>2. Uaminifu kwa Kristo kama ulivyoonyeshwa na Paulo ni muhimu sana. |
| **TOA UTANGULIZI** | Waulize wanafunzi kwanini wanafikiri Biblia ni muhimu sana. (Kumbuka Neno la Bwana limetajwa mara ngapi katika Neno la Biblia kwenye Funzo hili.)<br>Wape wanafunzi utangulizi wa wazo kwamba mkazo mkuu wa Biblia ni ujumbe wa Kristo ambao ni kwa ajili ya watu wote. Wakumbushe kuwa Wakristo wametoka kwenye tamaduni tofauti. | Waulize wanafunzi kufafanua neno 'mwaminifu'. Waulize wanafunzi wafikirie mifano ya uaminifu wa kawaida, na watu wanaoonesha uaminifu. Fikiria kwa nini uaminifu ni muhimu sana. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Sasa Paulo anawasili Antiokia (Pisidia), ambapo baada ya ujumbe wake wa kwanza katika sinagogi alialikwa kurudi Sabato iliyofuata.<br>2. Sabato iliyofuata karibu mji wote ulihudhuria kumsikia Paulo jambo ambalo liliwafanya viongozi wa Kiyahudi waone wivu sana.<br>3. Paulo alisema kuwa kwa sababu walikuwa wamekataa Neno la Mungu, sasa angeenda kwa Mataifa kama ***Isaya 49: 6*** inavyosema.<br>4. Sisitiza kuhusu watu waliokuwa wanamsikiliza. ***(mistari 16, 42, 43 na 48)***<br>5. Elezea kwanini Injili ilihubiriwa kwanza kwa Wayahudi.<br>6. Fafanua jinsi Neno la Mungu linavyoenea. ***(mstari 49)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Paul and Barnabas in Antioch and Iconium (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Wakati ambapo Paulo na Barnaba walifika Ikonio Wayahudi na Watu wa mataifa wengi waliamini lakini Wayahudi wengine wakachochea upinzani.<br>2. Jiji liligawanywa kwa sababu ya Injili lakini wengine walipanga njama ya kuwapiga mawe Paulo na Barnaba kwa hivyo wakakimbilia Listra.<br>3. Hapa Mungu alimtumia Paulo kumponya mtu kiwete na matokeo yake ni kuwa, watu wa jiji hilo wakadhani kuwa wao ni miungu, na wakataka kuwatolea dhabihu.<br>4. Paulo na Barnaba waliwaambia umati wa watu kwamba walikuwa wanajaribu kuwatoa mbali na sanamu zao zisizo na maana na kuwapeleka kwa Mungu aliye hai. Wakaelezea yote ambayo Mungu anatupatia. ***(mstari wa 17)***<br>5. Wayahudi walikuja kutoka Antiokia na Ikonia na kushawishi umati wa watu wampige Paulo kwa mawe na wakamkokota nje ya mji, akidhaniwa kuwa amekufa. Ashukuriwe Mungu! Paulo alinusurika na siku iliyofuata walienda Derbe. Hapa idadi kubwa wakawa wanafunzi.<br>6. Kisha wakarudi Listra, Ikonio na Antiokia ili kuwatia moyo Wakristo, jambo hili pengine lilihatarisha maisha yao.<br>7. *Sisitiza Mungu ni nani.* ***(mistari ya 15-17)***<br>8. *Tafakari umuhimu wa uvumilivu - Kama ilivyokuwa kwa Paulo na Barnaba. Angalia kwa umakini* ***mstari wa 22.***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Paul and Barnabas in Antioch and Iconium (I)** |
| **REJELEA SOMO** | Rejelea somo kwa kuwauliza wanafunzi kuelezea jinsi ambavyo Mungu anamshinda Shetani kwenye somo tulilojifunza hivi karibuni. | Wape wanafunzi jaribio kuhusu funzo la leo kama njia ya kurejelea somo.<br>1. Kusudi la 'ishara na maajabu' katika ***mstari wa 3*** lilikuwa nini?<br>2. Je! Paulo na Barnaba walikuwa makini kuhusu uaminifu wao kwa Mungu katika kifungu hiki? Je! Mungu anatarajia tuyatoe maisha yetu kwa kazi yake? |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Fikiria kuhusu mwitikio wa ujumbe kuhusu Kristo kwa Watu wa Mataifa katika ***mstari wa 42 na 48***. Je, tunaweza kujifunza nini kutokana na jambo hili kuhusu mwitikio wetu kwa ujumbe wa Kristo?<br>2. Jifunze kuhusu kazi ya shirika au kikundi kimoja cha Wamishenari katika jitihada yao ya kupeleka ujumbe wa Kristo kwenye tamaduni zingine au watu wengine. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Katika vikundi, andika chemshabongo ya neno 'Mwaminifu' kulingana na maisha ya Kikristo.<br>2. Unda onyesho la ukuta ukizingatia jinsi ujumbe wa Kristo unavyopinga ibada yetu ya sanamu katika jamii ya leo. |

| | A10 – DARAJA LA 3<br>Somo la Kwanza – Safari za Paulo<br>Mada – Kuteseka kwa ajili ya Bwana | A10 – DARAJA LA 4<br>Funzo la Kwanza – Safari za Paulo<br>Mada – Paulo huko Filipi |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Matendo 14: 1-21***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Petro 4: 16***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Wakristo wakati mwingine huteseka kwa sababu ya imani yao na hawapaswi 'kukata tamaa' wakati mambo yanapokuwa magumu.<br>2. Wakristo wana imani kwa Mungu aliye hai ambaye ni Muumbaji anayetimiza mahitaji yetu. | **Neno la Biblia:** ***Matendo 16: 9-40***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 16: 31***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ni muhimu kusikiliza na kutii uongozi wa Mungu.<br>2. Mungu hufungua mioyo ya watu na kwamba wokovu kwa mtu yeyote ni kupitia kwa Bwana Yesu Kristo. |
| **TOA UTANGULIZI** | Chunguza na wanafunzi kwanini ni muhimu kumwamini Mungu Muumbaji. Zingatia wazo la uwajibikaji mbele za Mungu. | Uliza swali kwa nini sisi sote tunahitaji wokovu wa Mungu. Elezea asili ya wokovu wa Mungu na jinsi tunavyookolewa kwa kuamini kile Mungu alichofanya kupitia kwa Bwana Yesu na sio kwa matendo yetu wenyewe. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Wakati Paulo na Barnaba walipofika Ikonio Wayahudi na Wamataifa wengi waliamini lakini baadhi ya Wayahudi wakachochea upinzani.<br>2. Jiji liligawanyika kwa sababu ya Injili lakini baadhi walikuwa wamefanya njama ya kuwapiga mawe Paulo na Barnaba hivyo basi wakalazimika kukimbilia Listra.<br>3. Hapa Mungu alimtumia Paulo kumponya mtu kiwete na matokeo yake ikawa, watu wa jiji hilo wakadhani kuwa wao ni miungu, na wakataka kuwatolea dhabihu.<br>4. Paulo na Barnaba wakauambia umati wa watu kuwa walikuwa wanajaribu kuwatoa kutoka kwenye sanamu zisizo na maana na kuwapeleka kwa Mungu aliye hai. Wakaelezea yote ambayo Mungu anatupatia.<br>5. Wayahudi walikuja kutoka Antiokia na Ikonio na kushawishi umati wa watu kumpiga Paulo kwa mawe na akakakokotwa hadi nje ya mji akidhaniwa amekufa.<br>6. Mungu ashukuriwe Paul alinusurika na kesho yake wakaenda Derbe.<br>7. Sisitiza Mungu ni nani. (mistari ya 15-17)<br>8. Tafakari umuhimu wa uvumilivu - Kama ilivyokuwa kwa Paulo na Barnaba.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Paul and Barnabas in Lystra and Derbe (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Kwa uwazi, Paulo alielekezwa asiende sehemu zingine za Asia, lakini alipokea maono usiku mmoja akiambiwa aende Makedonia (Ulaya).<br>2. Elezea matukio ambayo yalipelekea Injili kwenda Ulaya. ***(mstari wa 9)***<br>3. Huko Filipi alikutana na kikundi cha wanawake wakiomba karibu na mto. Alikuwemo Lidia.<br>4. Elezea nini maana ya Mungu kufungua moyo wa Lidia. ***(mstari wa 14)***<br>5. Wakati Paulo alipomwamuru pepo mbaya atoke kwa msichana mwenye pepo wa uaguzi, yeye na Sila wakaishia gerezani.<br>6. Kulikuwa na tetemeko la ardhi na wafungwa wote wakawa huru. Mlinzi wa gereza alikuwa karibu kujiua lakini Paulo alimhakikishia kwamba hakuna mtu aliyetoroka.<br>7. Elezea vizuri, swali ambalo msimamizi wa gereza aliuliza na jibu ambalo Paulo alimpa. ***(Matendo 16: 31)***<br>8. Sisitiza umuhimu wa Bwana Yesu Kristo kwa wokovu.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Paul and Silas travel to Philippi and Paul and Silas in prison (I)** |
| **REJELEA SOMO** | Unganisha somo la Biblia na ***Kutoka 20: 1-6***. Wasaidie wanafunzi kuelewa uhalisia wa Mungu Aliye hai. Fikiria ni aina gani ya sanamu kwenye jamii ya leo zinaweza kuwa katikati yetu sisi na Mungu. | Rejela somo kwa kutumia maswali yafuatayo:<br>1. Elezea matukio yaliyotokea mlinzi wa gereza alipookoka.<br>2. Je! Ni nini asili na vigezo vya ubatizo katika kifungu hiki? ***(mistari 15, 31-33)*** |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Fikiria juu ya wazo la uwajibikaji mbele za Mungu na jinsi hali hiyo inavyotupa changamoto? Je! Hali hiyo inapaswa kuleta mabadiliko gani katika maisha yetu ya Kikristo?<br>2. Je! ***Mstari wa 15*** unatufundisha nini kuhusu ibada ya 'shujaa'? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kuelewa wazo kwamba wokovu ni kwa neema ya Mungu tu.<br>2. Umuhimu wa ubatizo wa waumini. |

| | A10 – DARAJA LA 3<br>Somo la Pili – Safari za Paulo<br>Mada – Rafiki wa Maisha | A10 – DARAJA LA 4<br>Funzo la Pili – Safari za Paulo<br>Mada – Paulo akiwa Thesalonike na Beroya |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Matendo 16: 1-3; 2 Timotheo 1: 1-5***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***2 Timotheo 3: 15***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Kusoma na kujua Maandiko hutufanya tuwe wenye busara kwa wokovu.<br>2. Ni muhimu kuwa na marafiki Wakristo na kuombeana. | **Neno la Biblia:** ***Matendo 17: 1-14***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 17: 11***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu ndiye Kristo, aliyetabiriwa katika Agano la Kale, na ambaye kifo chake na ufufuo wake ulikuwa wa lazima.<br>2. Ni muhimu kuchunguza Maandiko ili kujua imani ya Kikristo ni nini. |
| TOA UTANGULIZI | Jadili ni vitu gani vinaathiri zaidi maisha yetu kwa mema au mabaya. Chunguza pamoja na wanafunzi umuhimu wa kuwa na ushawishi wa Kikristo maishani mwetu. Zungumza kuhusu nani wamekushawishi katika imani ya Kikristo na wamekushawishi kwa njia gani. | Waulize wanafunzi waseme nani wanawachukulia kama watu muhimu na kwanini wanadhani ni wa muhimu. Elezea kwamba ujumbe wa Kikristo ni juu ya mtu wa kipekee. Waalike wasikilize ujumbe kama unavyosomwa katika Matendo 17: 1-14. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Elezea kuhusu familia ya Timotheo.<br>2. Elezea jinsi ambavyo bibi na mama yake Timotheo walikuwa watu wa muhimu kwa imani yake.<br>3. Fikiria kuhusu jinsi ilivyo muhimu kuthamini familia ya Kikristo.<br>4. Tafakari ni kwanini Paulo aliamini ilikuwa lazima kumtahiri Timotheo. Je! tunajifunza nini kutokana na jambo hili?<br>5. Kisha Timotheo akaanza kusafiri pamoja na Paulo na akawa msaada mkubwa kwake.<br>6. Angalia maneno ya Paulo kwa Timotheo katika barua yake aliyomwandikia. ***(2 Timotheo 1: 3-5)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha: - Hakuna vielelezo vinavyofaa vya FBI.** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Paulo alisafiri kutoka Filipi kwenda Thesalonike ambako alihubiri katika sinagogi.<br>2. *Elezea ujumbe ambao Paulo alihubiri katika sinagogi huko Thesalonike. Pia elezea jina 'Kristo' linamaanisha nini, yaani maana yake, Mwokozi aliyetiwa mafuta na Mungu.*<br>3. *Fikiria kuhusu maana ya ujumbe.*<br>4. *Tafakari maneno yafuatayo: "Hawa walioupindua ulimwengu."* ***(mstari wa 6)***<br>5. Paulo na Sila, kwa mara nyingine tena, walilazimika kuondoka kwa haraka wakati wa usiku kisha wakaenda Beroya.<br>6. Wayahudi huko Beroya walikuwa tofauti sana na wale wa Thesalonike, na walijifunza Maandiko kila siku. ***(mistari ya 11-12)***<br>7. Walakini kulikuwa na upinzani zaidi na Paulo alilazimika kupelekwa Athene.<br>8. Linganisha upinzani ambao Paulo na Sila waliupata na upinzani ambao Wakristo wa leo wanakabiliana nao kwenye imani yao.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Paul in Thessalonica and Berea (I)** |
| REJELEA SOMO | Jifunze Mstari Muhimu na ujadili pamoja na wanafunzi darasani jinsi ambavyo mstari huu unatoa muhtasari wa somo la leo. | Soma ***Yoshua 1: 8*** na uilinganishe na Mstari Muhimu. ***(Matendo 17: 11)*** Zipo changamoto gani kwetu kama Wakristo? |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kuelewa umuhimu wa kuwa na marafiki wa Kikristo.<br>2. Kutafuta urafiki wa Kikristo.<br>3. Kuwaombea marafiki na jamaa zetu kwamba wawe na imani kwa Bwana Yesu. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Umuhimu wa kusoma Biblia na kuweka msingi wa maoni yetu na mtazamo wetu katika Biblia. (angalia Mstari Muhimu)<br>2. Jinsi ambavyo kuamini Yesu ni Mfalme kunapaswa kuleta tofauti katika maishani yetu. |

| | A10 – DARAJA LA 3<br>Somo la Tatu – Safari za Paulo<br>Mada – Paulo Gerezani | A10 – DARAJA LA 4<br>Funzo la Tatu – Safari za Paulo<br>Mada – Paulo akiwa Athene na Korintho |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Matendo 16: 16-34***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 16: 31***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Wokovu unapatikana kupitia Bwana Yesu Kristo.<br>2. Wale ambao wameokolewa wanapaswa kubatizwa. | **Neno la Biblia:** ***Matendo 17: 15-34; 18: 1-18***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 17: 30-31***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Toba imeamriwa na Mungu.<br>2. Mungu atahukumu ulimwengu. |
| **TOA UTANGULIZI** | Shirikisha wanafunzi hadithi kuhusu kuokolewa. Tumia hadithi hiyo kuelezea maana ya maneno: 'kuokolewa', 'Mwokozi', 'wokovu'. Wahimize wanafunzi kushirikisha kama wanajua wokovu katika maisha yao. | Waulize wanafunzi watoe ufafanuzi wa maana ya toba. Tumia ***1 Wathesalonike 1: 9*** kama njia ya kuelezea dhana ya 'toba'. Zingatia wazo la kumgeukia Mungu kama Mwokozi na kwamba hii inajumuisha kuacha njia yetu ya zamani ya kimaisha. Shuhuda za watu waliobadilishwa na Injili zinapaswa kutolewa ili kuongeza uzito wa maana ya toba. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Elezea matukio ambayo yalipelekea Injili kwenda Ulaya. ***(mstari wa 9)***<br>2. Huko Filipi alikutana na kikundi cha wanawake wakiomba karibu na mto. Mmoja wao alikuwa Lidia.<br>3. Elezea nini maana ya Mungu kufungua moyo wa Lidia. ***(mstari wa 14)***<br>4. Wakati Paulo alipomwamuru pepo mbaya atoke kwa msichana mwenye pepo la uaguzi, yeye na Sila waliishia kwenye gerezani.<br>5. Kulikuwa na tetemeko la ardhi na wafungwa wote wakawa huru. Mlinzi wa gereza alikuwa karibu kujiua lakini Paulo akamhakikishia kwamba hakuna mtu aliyetoroka.<br>6. Elezea wazi swali ambalo mlinzi wa gereza aliuliza na jibu ambalo Paulo alimpa. ***(Matendo 16: 31)***<br>7. *Sisitiza mamlaka yaliyopo kwa Jina la Yesu.* ***(mstari wa 18)***<br>8. *Elezea kwamba wakati mwingine Wakristo wanaweza kuonewa/ kutendewa mambo ambayo sio haki.* ***(mstari wa 23)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI- Paul and Silas travel to Philippi and Paul and Silas in prison (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Paulo amewasili Athene na anazungukazunguka akiwasubiria wenzake pia waje Athene. Anakasirishwa na idadi ya sanamu alioiona.<br>2. Paulo akaanza kuhubiri juu ya Yesu katika soko na katika sinagogi.<br>3. Paulo alipelekwa mahali muhimu na mwafaka ambapo aliombwa kuelezea mafundisho haya mapya.<br>4. Paulo alizungumza kuhusu Mungu Muumbaji mkuu aliyeumba ulimwengu, lakini pia alisema Yeye yupo karibu na kila mmoja wetu. Alisema pia kwamba Mungu atahukumu ulimwengu kupitia mtu aliyemteua ambaye alimfufua katika wafu.<br>5. Waliposikia habari za ufufuo wengi walimdhihaki, lakini wengine waliamini. Mara Paulo akaenda Korintho.<br>6. Hapa alikutana na Akila na Prisila ambao walikuja kuwa wasaidizi wake. Alikaa Korintho kwa miezi 18 na watu wengi wakawa waumini.<br>7. ***Matendo 18: 9*** - Mungu alimhakikishia kwamba atakuwa salama huko Korintho.<br>8. *Sisitiza kile Paulo anachofundisha kuhusu Mungu katika* ***mistari 24-31***.<br>9. *Fikiria kuhusu asili ya hukumu.*<br>10. *Tafakari jinsi watu walivyoitikia ujumbe wa Paulo huko Athene na Korintho.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Paul in Athens and Paul in Corinth (I)** |
| **REJELEA SOMO** | Andaa bodi ya grafiti kwenye habari ya Paulo na Sila huko Filipi. | Linganisha jinsi ambavyo Paulo alihubiri huko Athene na huko Korintho. Je! Kulikuwa na tofauti yoyote kwa namna aliyohubiri kwenye maeneo haya mawili? Je, ni kwa nini? |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kuhusu umuhimu wa kujua wokovu kupitia kwa Bwana wetu Yesu Kristo.<br>2. Kuhusu kutambulisha hadharani uhusiano wetu na Kristo kwa njia ya Ubatizo. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kuhusu umuhimu wa toba na jinsi Mkristo anavyotakiwa kumgeukia Mungu kila siku na kuwa mbali na dhambi.<br>2. Kuhusu kuwaambia wengine juu ya Injili na jinsi Mungu atakavyouhukumu ulimwengu siku moja. |

<table>
<tr><th></th><th>A10 – DARAJA LA 3<br>Somo la Nne – Safari za Paulo<br>Mada – Mji wa Athene</th><th>A10 – DARAJA LA 4<br>Funzo la Nne – Safari za Paulo<br>Mada – Paulo akiwa Efeso</th></tr>
<tr><td></td><td>Neno la Biblia: Matendo 17: 10-34<br><br>Mstari Muhimu: Matendo 17: 30<br><br>Tunajifunza kuwa:<br>1. Mungu ni Mungu Aliye Hai na aliyeumba dunia.<br>2. Mungu anaamuru watu wote watubu.<br>3. Mungu atahukumu ulimwengu kwa haki.</td><td>Neno la Biblia: Matendo 19: 1-41<br><br>Mstari Muhimu: Ephesians 2: 8-9<br><br>Tunajifunza kuwa:<br>1. Neno la Mungu na kazi ya Mungu ikaenea huko Efeso.<br>2. Jina la Bwana Yesu likatukuzwa.</td></tr>
<tr><td>TOA UTANGULIZI</td><td>Waulize wanafunzi, je, wanaelewa nini kuhusu sanamu? Waambie waelezee maana ya sanamu. Jadiliana nao amri mbili za kwanza kwenye Kutoka 20. Tumia 1 Wathesalonike 1: 9 kuelezea maana ya toba.</td><td>Rejelea somo ulilojifunza kwenye Funzo la tatu. Fikiria kuhusu toba na inaweza kumaanisha nini katika maisha ya kila siku. Endeleza wazo kwamba toba huleta badiliko la mtindo wa maisha. Fafanua Matendo 19: 18-20.</td></tr>
<tr><td>KAMILISHA</td><td>Wasilisha Habari ya Biblia<br><br>Jadili na uelezee:<br>1. Paulo amewasili Athene na anazungukazunguka akisubiria wenzake pia waje Athene. Anachukizwa na idadi ya sanamu alizoziona.<br>2. Paulo akaanza kuhubiri kuhusu Yesu katika soko na katika sinagogi.<br>3. Paulo alipelekwa mahali muhimu na mwafaka ambapo aliombwa kuelezea mafundisho hayo mapya.<br>4. Paulo alizungumza kuhusu Mungu Muumbaji mkuu aliyeumba ulimwengu, lakini pia alisema Yeye yupo karibu na kila mmoja wetu. Alisema pia kwamba Mungu atahukumu ulimwengu kupitia mtu aliyemteua ambaye alimfufua katika wafu.<br>5. Waliposikia habari za ufufuo wengi walimdhihaki lakini wengine waliamini. Mara Paulo akaenda Korintho.<br>6. Sisitiza kile ambacho Paulo alifundisha kumhusu Mungu. (mistari ya 24 -31)<br>7. Sisitiza umuhimu wa ufufuo wa Yesu. (mstari wa 31)<br>8. Jadili mwitikio wa mahubiri ya Paulo. (mistari ya 32-34)<br><br>Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.<br>Kamilisha Somo la Nne.<br>Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Paul in Athens (I)</td><td>Wasilisha Habari ya Biblia<br><br>Jadili na uelezee:<br>1. Sasa Paulo anahamia Efeso ambapo anakutana na wanafunzi wengine ambao hawajampokea Roho Mtakatifu.<br>2. Elezea kwanini ilikuwa ni lazima kwa Paulo kubatiza wanafunzi wa Yohana.<br>3. Baada ya Wayahudi wa sinagogi kukataa mahubiri ya Paulo, Paulo alihamia kwenye ukumbi wa mafunzo na kukaa huko kwa miaka miwili.<br>4. Mungu alifanya miujiza ya ajabu kwa kumtumia Paulo. (mstari wa 11) Kutokana na nguvu ya Roho Mtakatifu iliyodhihirika kupitia Paulo, watu wengi wakaamini na kutangaza imani yao waziwazi. Elezea walichofanya.<br>5. Elezea kwa kifupi matukio yaliyopelekea kutokea vurugu huko Efeso. (mistari ya 23-41)<br>6. Elezea nini maana ya neno 'Ufalme wa Mungu'. (mstari wa 8)<br>7. Eleza jinsi Neno la Mungu lilivyoshinda huko Efeso. (mstari wa 20)<br>8. Jadili jinsi Wakristo wapya wanavyoweza kushughulikia mazoea na tabia zao za zamani.<br><br>Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.<br>Kamilisha Funzo la Nne.<br>Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Paul in Ephesus, and Silversmiths in Ephesus riot against the Way (I)</td></tr>
<tr><td>REJELEA SOMO</td><td>Katika vikundi, jadili jinsi ujumbe wa Kikristo unavyoweza kuwasilishwa katika namna inayoleta changamoto katika jamii yako. Kuza jambo hili kupitia tukio la kiinjilisti.</td><td>Chora ramani ya akili inayoitwa 'Injili yafika Efeso'. Andika makala ya gazeti kuhusu matukio yaliyoelezewa katika Matendo 19.</td></tr>
<tr><td>LIISHI SOMO</td><td>Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:<br>1. Kuhusu toba ya kibinafsi. Inamaanisha nini kumgeukia Mungu kutoka dhambini?<br>2. Kuhusu umuhimu wa uinjilisti. Tunawezaje kushirikisha wengine ujumbe wa Injili?</td><td>Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:<br>1. Imani ya Kikristo inajulikana kama 'Njia'. (mstari 9) Je! hii inamaana gani? Je! Hii inatupa changamoto ipi?<br>2. Je! Tunaweza kujifunza somo gani la kivitendo kuhusu majukumu yetu kwa umma kutokana na vitendo vya karani wa mji katika mstari wa 35-41?</td></tr>
</table>

<table>
<tr><th></th><th>A11 – DARAJA LA 3<br>Somo la Kwanza – Safari za Paulo<br>Mada – Kushiriki na wengine</th><th>A11 – DARAJA LA 4<br>Funzo la Kwanza – Majaribu ya Paulo<br>Mada – Yerusalemu na Umati wa Watu</th></tr>
<tr><td></td><td>Neno la Biblia: Matendo 18: 1-11<br><br>Mstari Muhimu: Matendo 18: 9-10<br><br>Tunajifunza kuwa:<br>1. Ujumbe wa Paulo popote alipoenda ni kwamba Yesu ndiye Kristo.<br>2. Mungu alikuwa na Paulo na alimtia moyo katika maono.</td><td>Neno la Biblia: Matendo 21: 17-40; 22: 1-30<br><br>Mstari Muhimu: Matendo 22 : 14 & 15<br><br>Tunajifunza kuwa:<br>1. Baada ya Paulo kukamatwa Hekaluni, alitoa ushuhuda wake mbele za umati wa watu.<br>2. Wayahudi walichukia ule uhalisia kwamba, Watu wa Mataifa walikuwa wamepokea na kuitikia Injili.<br>3. Paulo anadhihirisha uraia wake wa Kirumi wakati walipoanza kumpiga.</td></tr>
<tr><td>TOA UTANGULIZI</td><td>Wasimulie wanafunzi habari yako binafsi ya jinsi ambavyo Mungu alikutia moyo. Jadili maana na umuhimu wa kutia moyo katika maisha ya Kikristo. Waombe wanafunzi watoe mifano ya hali za kutiwa moyo waliopata.</td><td>Kwa kifupi toa utangulizi wa upinzani ambao Paulo alikabiliana nao alipofika Yerusalemu.<br>Kwa kutumia tovuti ya Voice of the Martyrs (au chanzo kingine), toa mifano ya Wakristo waliomtangaza Kristo na hawakuogopa kuteseka. Waulize wanafunzi, je, ni kwanini Mkristo afanye hivi?</td></tr>
<tr><td>KAMILISHA</td><td>Wasilisha Habari ya Biblia<br><br>Jadili na uelezee:<br>1. Paulo anawasili Korintho, na kukutana na Akila na Prisila ambao wanakuwa wasaidizi wake.<br>2. Kama kawaida kila Sabato anaenda kwenye sinagogi kuwashawishi Wayahudi kuwa Yesu ndiye Masihi ambaye wamekuwa wakimngojea.<br>3. Wayahudi walipokuwa wakatili, Paulo anaenda kwenye mlango wa pili na sasa anahubiria zaidi kwa Watu wa Mataifa. Wengi wanaamini na kubatizwa.<br>4. Matendo 18: 9 - Mungu alimhakikishia Paulo kwamba, akiwa huko Korintho, atakuwa naye na atakuwa salama. Elezea kwa jinsi gani jambo hili ni la kutia moyo sana kwa Paulo.<br>5. Sisitiza jinsi ambavyo Paulo alieneza ujumbe. (mstari wa 4 & 11)<br>6. Tafakari jinsi ambavyo Neno la Mungu lilienea huko Korintho na umuhimu wa ubatizo.<br><br>Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.<br>Kamilisha Somo la Kwanza.<br>Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Paul in Athens and Paul in Corinth (I)</td><td>Wasilisha Habari ya Biblia<br><br>Jadili na uelezee:<br>1. Paulo anawasili Yerusalemu na kwenda Hekaluni. Alishitakiwa kimakosa kwamba amemuingiza mtu wa Mataifa ndani ya hekalu na jambo hili likasababisha vurugu.<br>2. Aliokolewa na jemadari wa Kirumi na kuruhusiwa kuongea na umati wa watu akiwa kwenye madaraja ya ngome.<br>3. Paulo alitoa ushuhuda wazi kabisa. (Matendo 22: 1-21) Aliposema kwamba alikuwa ametumwa kwa Mataifa, ghafla kukatokea vurugu nyingine.<br>4. Alipelekwa ndani ya ngome na wangalimpiga kama asingeeleza kwamba alikuwa raia wa Rumi na asingeweza kupigwa hadi atakapopatikana na kosa la jinai.<br>5. Sisitiza kwa nini Paulo alienda Hekaluni.<br>6. Sisitiza pia hali ya uongofu wa Paulo.<br>7. Elezea kwa nini umati ulikuwa na uhasama na Paulo.<br><br>Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.<br>Kamilisha Funzo la Kwanza.<br>Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Paul arrested in Jerusalem</td></tr>
<tr><td>REJELEA SOMO</td><td>Rejelea habari hii kwa njia ya maswali.</td><td>Anzisha mjadala hapo darasani kuona kama Paulo alitumia busara kuingia Hekaluni alipokuwa Yerusalemu.</td></tr>
<tr><td>LIISHI SOMO</td><td>Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:<br>1. Soma Zaburi ya 23 na ufikirie jinsi ambavyo ahadi ya uwepo wa Mungu inatutia moyo kama Wakristo.<br>2. Fikiria kuhusu namna ambazo tunaweza kuwatia moyo watu kwa kuwa pamoja nao. Lifanyie kazi jambo hili.</td><td>Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:<br>1. Wakristo wanakamatwa kila siku ulimwenguni. Panga muda wa maombi ya kila siku, ukiwafikiria Wakristo wanaoteswa.<br>2. Waelekeze wanafunzi watafakari kuhusu wiki yao na kugundua fursa ambazo wanaweza kuwa wamezipoteza katika kumshuhudia/ kumtangaza Kristo. Waambie wamuombe Mungu msaada na ujasiri wa kuwa waaminifu katika ushuhudiaji kwenye siku zijazo.</td></tr>
</table>

| | **A11 – DARAJA LA 3**<br>**Somo la Pili – Safari za Paulo**<br>**Mada – Mpango wa kumuua** | **A11 – DARAJA LA 4**<br>**Funzo la Pili – Majaribu ya Paulo**<br>**Mada – Kaisaria na Maliwali (Magavana)** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Matendo 23: 10-24; 24: 22-27***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Zaburi 18: 30***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu alimtia moyo Paulo wakati ambapo Wayahudi walijaribu kumuua.<br>2. Paulo aliendelea kuhubiri Neno la Mungu kwa uaminifu hata akiwa mfungwa. | **Neno la Biblia:** ***Matendo 23: 23-26; 24: 1-27; 25: 1-12***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Petro 3: 15***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Paulo alichukuliwa kwenda Kaisaria kwa ajili ya usalama na mwishowe akakata rufaa kwa Kaisari.<br>2. Katika majaribu mbali mbali aliyokuwa akikabiliana nayo, Paulo alihubiri kuhusu haki, kuwa na kiasi na hukumu itakayokuja. (24: 25) |
| **TOA UTANGULIZI** | Wakumbushe wanafunzi kuhusu nguvu ya Ufalme wa Kirumi katika siku za Paulo. Elezea ngao ni nini. Onesha vielelezo/picha ya askari wa Kirumi akiwa na ngao kutoka kwenye ulimwengu wa kale wa Kirumi na Kigiriki. Elezea jinsi ambavyo BWANA ni ngao kwa watu wake. Wahimize wanafunzi kujifunza Mstari Muhimu - Zaburi 18: 30. | Husianisha habari ya Martin Luther na msimamo wake kwa Kristo kwenye Baraza la Kifalme (Imperial Diet of Worms kwa Lugha ya Kiingereza) mnamo 1521. Tafakari maelezo haya ya Luther huko Worms: "Isipokuwa nina hakika na Maandiko na sababu dhahiri ... dhamiri yangu ni mateka kwa Neno la Mungu. Siwezi na sitaacha imani niliyo nayo, kwa kuwa kupingana na dhamiri sio sawa wala salama. Mungu nisaidie. Amina."<br>Tumia hii kama utangulizi wa hali iliyompata Paulo. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Paulo ameletwa mbele ya Baraza la Wayahudi wa Kidini. (Sanhedrini au Sanhedrin kwa Lugha ya Kiingereza)<br>2. Kulikuwa na ugomvi mkubwa kwa sababu Paulo alitaja ufufuo; baadhi waliamini lakini wengine hawakuamini hivyo kukawa na makelele mengi. ***(Matendo 23: 9)***<br>3. Maisha ya Paulo yalikuwa hatarini kwa hivyo aliokolewa na Jemadari wa Kirumi.<br>4. Usiku huo Bwana alisimama karibu na Paulo akamwambia awa na moyo mkuu kwa sababu atakwenda Rumi ili kueneza Injili.<br>5. Wayahudi wengine walijifunga kiapo kwamba hawatakula wala kunywa hadi Paulo afe, na walipanga njama ya kumuua.<br>6. Kwa bahati nzuri mpwa wa Paulo aliposikia habari ya njama hiyo, akamwambia Jemadari na akamfanya Paulo alindwe na kupelekwa Kaisaria.<br>7. Paulo alilazimika kuenda mbele ya Liwali wa Rumi, Festo, na kwa mara nyingine tena akaelezea Injili.<br>8. *Sisitiza ujumbe ambao Paulo alimhubiria Feliki na umuhimu wake kwetu leo.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Paul arrested in Jerusalem, and Paul's trial before Festus (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Paulo anapelekwa Kaisaria kwa usalama wake mwenyewe na kuletwa kwa Liwali Feliki.<br>2. Kisha kukawa na mashtaka mbele ya Feliki wakati ambapo viongozi wa Kiyahudi walimshtaki kwa kunajisi Hekalu na kusababisha vurugu.<br>3. Paulo anawajibu washitaki wake, na Feliki anakuwa na mahojiano mengine na Paulo na Paulo anaongea wazi juu ya imani katika Kristo Yesu. ***(Matendo 24: 24)***<br>4. Paulo aliachwa gerezani kwa miaka miwili mpaka Liwali mwingine alipokuja.<br>5. Sasa Paulo anajitokeza mbele ya Festo na tena viongozi wa Kiyahudi wanakuja na kumshtaki. Paulo anakataa kwenda Yerusalemu na kukata rufaa kwa Kaisari na Festo anasema atakwenda Rumi.<br>6. Elezea jinsi ambavyo Paulo anajitetea mbele ya Feliki.<br>7. *Tafakari ni kwanini Feliki alitetemeka aliposikia mahubiri ya Paulo.* ***(Matendo 24: 25)***<br>8. *Fikiria ni kwa nini Paulo alikata rufaa kwa Kaisari na hii ilikuwa na maana gani.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Paul's trial before Festus (I)** |
| **REJELEA SOMO** | Andika maandishi kwenye kitabu chako cha kumbukumbu yenye kichwa: 'Kusubiri ahadi ya Mungu'. | Unda bodi ya Grafiti yenye kichwa 'Paulo aonesha msimamo wake kwa Yesu Kristo. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Fikiria juu ya ahadi ambayo Paulo alipewa na Mungu wakati wa usiku. Je! Kuna kitu au mtu yeyote angeweza kuzuia ahadi hii kutimia? Kwa namna gani jambo hili linatutia moyo leo?<br>2. Feliki alitetemeka na kuogopa kusikia Neno la Mungu. ***(Matendo 24:25)*** Je! Tunatetemeka tunaposikia Neno la Mungu? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Soma na utafakari ***2 Timotheo 2: 3***. Andika orodha ya magumu ambayo tumeyastahimili kama Wakristo. Pamoja na orodha hii, kumbuka jinsi ambavyo Mungu ametutia moyo na kutuwezesha kushinda nyakati ngumu.<br>2. Paulo alitumia uraia wake wa Rumi ili kusaidia kueneza Injili. Je! Tunaweza kutumia fursa za fadhila tulizonazo katika kueneza Injili? |

| | A11 – DARAJA LA 3<br>Somo la Tatu – Safari za Paulo<br>Mada – Mbele ya Mfalme | A11 – DARAJA LA 4<br>Funzo la Tatu – Majaribu ya Paulo<br>Mada – Kaisaria na Mfalme |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Matendo 25: 13-22; 26: 13-32***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 26: 22***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Sasa Paulo alilazimika kujitetea mbele ya Festo.<br>2. Mfalme Agripa alikuwa karibu kushawishika kuwa Mkristo. | **Neno la Biblia:** ***Matendo 25: 13-27; 26: 1-32***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 26: 28***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu anaingilia kati katika maisha ya Paulo. Festo anaona kuwa, Paulo hastahili kifo, na Agripa anafikiria kwamba anapaswa kuachiwa huru.<br>2. Paulo anatangaza wazi ujumbe wa Injili na anajaribu kumshawishi Agripa kuwa Mkristo. |
| TOA UTANGULIZI | Waulize wanafunzi kwa namna gani wanadhani mtu anaweza kuwa Mkristo? Elezea kwamba watu huwa Wakristo siyo kwa kulazimishwa. Jadili umuhimu wa kushawishi watu kuwa Wakristo. Kutokana na uzoefu wako, toa mifano ya jinsi ambavyo, kwa wakati mwingine, watu hulazimishwa kufanya vitu lakini hawana shauku navyo na hawaviamini pia. | Zungumza kuhusu aina ya upinzani ambao tunaweza kukabiliana nao katika imani yetu ya Kikristo. Je, wanafunzi wangewezaje kukabiliana na hali hiyo?<br>Tafakari kuhusu ahadi walizopewa wanafunzi wa Kristo katika Luka 21: 12-15. Fikiria namna ambavyo ahadi hizi zingetimizwa katika funzo hili. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Paulo amekuwa gerezani kwa miaka miwili. Sasa kuna Liwali mpya kwa jina Festo. Wayahudi walimtaka amlete Paulo Yerusalemu kwa ajili ya kesi, lakini Paulo akasema anataka kushtakiwa kule Rumi.<br>2. Mfalme Agripa na mkewe Bernike wanawasili Kaisaria na wanataka kusikia habari ya mfungwa Paulo.<br>3. Paulo analetwa mbele ya Agripa.<br>4. Paulo anamuelezea ushuhuda wa maisha yake. ***(Matendo 26: 1-23)***<br>5. Festo anasema ana wazimu! Agripa anakiri kwamba karibu ashawishike kuwa Mkristo. Wote wanakubali kwamba Paulo angeweza kuachiliwa huru lakini kwa kuwa alikuwa amekata rufaa kwa Kaisari ilibidi aende Rumi.<br>6. *Sisitiza utetezi wa Paulo mbele ya Festo na uamuzi wake.* ***(Matendo 26: 24-25)*** *Fikiria, pia jinsi ambavyo Paulo alijaribu kumshawishi Agripa kuwa Mkristo.*<br>7. *Fikiria jinsi ambavyo Paulo alijibu kukiri kwa Agripa.* ***(Matendo 26: 29)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Paul’s trial before Festus and Agrippa (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Paulo amekuwa gerezani kwa miaka miwili. Sasa kuna Liwali mpya kwa jina Festo. Wayahudi walimtaka amlete Paulo Yerusalemu kwa ajili ya kesi, lakini Paulo akasema anataka kushtakiwa kule Rumi.<br>2. Mfalme Agripa na mkewe Bernike wanawasili Kaisaria na wanataka kusikia habari ya mfungwa Paulo. Paulo analetwa mbele ya Agripa.<br>3. Paulo anamuelezea ushuhuda wa maisha yake. ***(Matendo 26: 1-23)***<br>4. Festo anasema ana wazimu! Agripa anakiri kwamba karibu ashawishike kuwa Mkristo. Wote wanakubali kwamba Paulo angeweza kuachiliwa huru lakini kwa kuwa alikuwa amekata rufaa kwa Kaisari ilibidi aende Rumi.<br>5. *Sisitiza utetezi wa Paulo mbele ya Festo na uamuzi wake.* ***(Matendo 26: 24-25)*** *Fikiria, pia jinsi ambavyo Paulo alijaribu kumshawishi Agripa kuwa Mkristo.*<br>6. *Fikiria jinsi ambavyo Paulo alijibu kukiri kwa Agripa.* ***(Matendo 26: 29)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Paul’s trial before Festus and Agrippa (I)** |
| REJELEA SOMO | Tengeneza bango la Kanisa lenye kichwa: 'Karibu kushawishika?' | Tafakari kuhusu funzo na ujadili kauli ifuatayo: 'Kushawishiwa ni bora zaidi kuliko kulazimishwa'. Je! Maelezo haya yanahusiana vipi na yale tuliyojifunza katika funzo hili? |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Fikiria jinsi ambavyo namna ya uinjilisti wa Paulo katika habari hii unatupa changamoto. Je, namna yetu ya kufanya uinjilisti ingebadilika vipi?<br>2. Andaa mdahalo wa darasani ambapo mwanafunzi mmoja anajaribu kumshawishi mwingine kuwa Mkristo. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Tofautisha mtazamo wa viongozi wa Kiyahudi na viongozi wa Kirumi katika ujumbe wa Injili kwenye kitabu cha Matendo. Je! Ni masomo gani tunaweza kujifunza kutokana na jambo hili kuhusu mwitikio wa watu kwenye ujumbe wa Injili?<br>2. Fikiria jinsi ambavyo somo la leo linatupa changamoto kuhusu namna tunavyotangaza ujumbe wa Injili. |

| | A11 – DARAJA LA 3<br>Somo la Nne – Safari za Paulo<br>Mada – Kuharibika kwa Merikebu | A11 – DARAJA LA 4<br>Funzo la Nne – Majaribu ya Paulo<br>Mada – Merikebu kuvunjika huko Mediterania/ Bahari ya Kati |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Matendo 27: 13-14, 20-44; 28: 1-9***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 27: 25***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu anaahidi kutusaidia katika kila hali tunayokabiliana nayo maishani.<br>2. Makusudi ya Mungu siku zote hutimia. | **Neno la Biblia:** ***Matendo 27: 1-44; 28: 1-10, 28-31***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 27: 24-25***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu anadhibiti kila hali tunayokabiliana nayo maishani na anaahidi kutusaidia kushinda hali hizo.<br>2. Kukataliwa kwa Injili na baadhi ya watu hutoa fursa kwa wengine kuisikia Injili. |
| TOA UTANGULIZI | Waulize wanafunzi kama wamewahi kuwa kwenye dhoruba. Hoji ujue jinsi walivyojisikia na kama waliomba wokovu wa Mungu. Tengeneza mazingira na husianisha hali yao na kuharibika kwa merikebu ya Paulo. | Jadili na wanafunzi suala la hofu. Waombe waeleze hofu zao zilizokuwa mbaya zaidi. Fikiria umuhimu wa ahadi za Mungu katikati ya hali za kutisha. ***(Zaburi 23: 4)*** |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Paulo sasa yuko safarini kwenda Rumi. Paulo aliwashauri wasiendelee na safari wakati wa msimu wa baridi lakini hakuna mtu aliyemsikiliza.<br>2. Kulikuwa na dhoruba kubwa ambayo ilidumu kwa siku nyingi. Usiku mmoja Paulo alipata maono na aliambiwa kwamba wote waliokuwa kwenye meli wangekuwa salama. Alimwambia kila mtu kuwa, yeye ana imani kwa Mungu na kila kitu kitatokea kama vile alivyokuwa ameambiwa.<br>3. Hatimaye walifika karibu na Melita, wakaiegesha merikebu nchi kavu na wote 276 wakafanikiwa kufika ufukweni salama.<br>4. Watu wa Melita walikuwa wakarimu sana kwao, na Paulo alifanya miujiza kadhaa kwenye kisiwa hicho.<br>5. *Sisitiza jinsi ambavyo Mungu alimtia moyo Paulo wakati wa dhoruba.*<br>6. *Sisitiza jinsi ambavyo Wakristo hawana kinga ya kuwafanya wasikutane na ugumu.*<br>7. *Fikiria jinsi ambavyo tunapopitia kwenye dhoruba za maisha, tunaweza pia kuhisi uwepo na nguvu za Bwana.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Paul is shipwrecked (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Paulo sasa yuko safarini kwenda Rumi. Tayari walikuwa wanapata shida huko Krete hivyo Paulo akawashauri wasiendelee na safari wakati wa msimu wa baridi lakini hakuna mtu aliyemsikiliza.<br>2. Kulikuwa na dhoruba kubwa ambayo ilidumu kwa siku nyingi. Mabaharia walipoteza tumaini la kuokolewa.<br>3. Usiku mmoja Paulo alipata maono ambapo aliambiwa kwamba wote waliokuwa kwenye meli wangekuwa salama. Alimwambia kila mtu kuwa, yeye ana imani kwa Mungu na kila kitu kitatokea kama vile alivyokuwa ameambiwa. Baada ya siku 14 bila kula chakula, Paulo akawahimiza kula na ndipo wakaanza kukaribia nchi kavu.<br>4. Mwishowe walifika karibu na Melita, wakaiegesha merikebu nchi kavu na wote 276 wakafanikiwa kufika ufukweni salama.<br>5. Watu wa Melita walikuwa wakarimu sana kwao, na Paulo alifanya miujiza kadhaa kwenye kisiwa hicho.<br>6. Hatimaye walifika Rumi, na Paulo akapewa kifungo cha nyumbani lakini akaitumia fursa hiyo kuwaambia watu kuhusu Bwana Yesu.<br>7. *Sisitiza jinsi Mungu alivyomtia moyo Paulo wakati wa dhoruba.*<br>8. *Sisitiza jinsi ambavyo Wakristo hawana kinga ya kuwafanya wasikutane na ugumu.*<br>9. *Fikiria jinsi ambavyo tunapopitia kwenye dhoruba za maisha, tunaweza pia kuhisi uwepo na nguvu za Bwana.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Paul is shipwrecked (I)** |
| REJELEA SOMO | Waambie wanafunzi wajichukulie kama wao ni Paulo. Waelekeze wamuandikie barua rafiki ambaye anakabiliwa na matatizo na waambie wahusianishe na jinsi Mungu alivyowatoa kwenye dhoruba njiani kwenda Rumi. Tumia hali hiyo kumtia moyo rafiki. | Soma ***2 Wakorintho 11: 21-33 na 2 Timotheo 4: 16-18***. Jadili na wanafunzi jinsi vifungu hivi viwili vinavyohusiana. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Waulize kwa namna gani habari ya kuharibika kwa merikebu ya Paulo kunatupa changamoto na kututia moyo.<br>2. Je! Ni masomo gani tunaweza kujifunza kutoka kwenye habari zingine za Biblia kuhusu Mungu alivyookoa watu katika nyakati ngumu, kwa mfano, Yusufu, Danieli, nk.<br>3. Tunga sala ya kumshukuru Mungu kwa ukuu wake katika maisha yetu. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Tafakari juu ya matukio katika maisha ya Paulo uliyojifunza na tambua jinsi ambavyo uaminifu wa Mungu unang’aa katika maisha yake.<br>2. Angalia kwenye kamusi maana ya neno 'uvumilivu'. Je! Kwa namna gani uvumilivu unaonekana katika maisha ya Paulo? Wape wanafunzi changamoto ya jinsi gani wanavyojilinganisha na Paulo kwenye suala hili. |

| | A12 – DARAJA LA 3<br>Somo la Kwanza – Krismasi ya Kwanza<br>Mada – Yasiyowezekana! | A12 – DARAJA LA 4<br>Funzo la Kwanza – Kuzaliwa kwa Mwokozi<br>Mada – Ujumbe wa Malaika |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Luka 1: 5-20, 57-66***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 1: 37***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Zakaria na Elisabeti walikuwa wanandoa wazee ambao walipata fursa ya Mungu kujibu sala zao.<br>2. Hakuna kisichowezekana kwa Mungu. | **Neno la Biblia:** ***Mathayo 1: 18-25 & Luka 1: 26-38***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 1: 21***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Kuzaliwa kwa Yesu kulitabiriwa kwa usahihi na malaika ambaye alimwambia baba mtarajiwa mambo muhimu kuhusu maisha yake.<br>2. Mariamu pia aliambiwa kwamba atapata mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. |
| TOA UTANGULIZI | Zungumza jinsi ambavyo nyakati zingine watu wanatakiwa kungojea ili kumuone Mungu akijibu maombi yao. Elezea hali ya Zakaria na Elisabeti na jinsi walivyotakiwa kungojea muda mrefu sana ili maombi yao yajibiwe kiasi cha kuonekana kabisa kuwa haiwezekani. | Fikiria juu ya njia ambazo matukio makubwa hutangazwa na kuonekana ulimwenguni pote, mara tu yanapotokea. Walakini hakuna mtu anayeweza kuyatabiri kwa usahihi au kujua nini kitatokea kabla ya tukio. Lakini Mungu anaweza! Wote wawili, Yusufu na Mariamu walipewa ujumbe kutoka kwa Mungu kuhusu kuzaliwa kwa Bwana Yesu, kabla hajazaliwa. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Elezea kwamba Zakaria na Elisabeti walitaka kuwa na watoto. Wakumbushe wanafunzi kuhusu aibu na maumivu waliyopata wanandoa huko Mashariki ya Kati kwenye nyakati za Biblia ikiwa mtu hakupata watoto.<br>2. Zakaria alibahatika, kama kuhani kufanya kazi Hekaluni.<br>3. Malaika akamtokea Zakaria naye akaogopa. Kisha malaika akamwambia kuwa Elisabeti atapata mtoto wa kiume ambaye atakuwa mkuu machoni pa Bwana, naye atatayarisha watu walioandaliwa kwa ajili ya Bwana. ***(Luka 1: 17)***<br>4. Zakaria anasema kwamba wao ni wazee sana kuweza kupata watoto. Malaika anasema kwamba, kwa sababu hajaamini Neno la Bwana hataweza kuongea hadi jambo hili litakapotokea.<br>5. Wakati mtoto amezaliwa Elisabeti anasema ataitwa Yohana na Zakaria anathibitisha hili kwa maandishi. Mara tu anapofanya hivyo, anaweza kuongea na anajazwa Roho Mtakatifu na kutabiri yote ambayo Yohana atayafanya.<br>6. *Fikiria kuhusu majirani walivyochukulia mambo haya, nk* ***(Luka 1: 65-66)***<br>7. *Tofautisha majibu ya Elisabeti katika ujumbe wa malaika na majibu ya Zakaria. Tunaweza kujifunza nini kwa hili?*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – The birth of John the Baptist (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mariamu na Yusufu walikuwa wachumba. Halafu Mariamu anapokea ujumbe kutoka kwa malaika kwamba atajifungua mtoto wa kiume, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.<br>2. Yusufu anaposikia hivi anataka kumwacha kwa siri. Walakini katika ndoto anaambiwa kuhusu kuzaliwa kwa Mtoto, sababu ya kuzaliwa kwake, na unabii ambao utatimizwa wakati wa kuzaliwa Kwake.<br>3. Yusufu na Mariamu wote waliamini ujumbe walioupokea, na kama Yusufu alivyoelekezwa alimpa mtoto jina la Yesu "kwa sababu atawaokoa watu Wake na dhambi zao".<br>4. *Fikiria kuhusu maswali haya matatu: a) Kwanini Yesu alichukuliwa mimba kwa njia ya kimiujiza na kwa Roho Mtakatifu na sio kwa njia ya kawaida? b) Kwanini Mariamu na Yusufu walichaguliwa kuwa wazazi wake wa kidunia? (Angalia orodha ya vizazi vyao-Mathayo 1 na Luka 3) c) Kwa nini Mungu alichagua kumtuma Mwanae wa pekee ulimwenguni?*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – The birth of Jesus (I)** |
| REJELEA SOMO | Chini ya kichwa cha "Lisilowezekana limewezekana" ruhusu wanafunzi kuandika mambo ambayo mwishowe yalitokea kweli (hasa mifano kutoka kwenye Biblia) ingawa walidhani hayawezekani. Andika hapo chini: Asante Mungu! | Je! Unaweza kupata nini kutoka kwenye mafunzo ya leo? Je, unaweza kutumia vipi ulilolipata katika maisha yako? Kuja kwa Bwana Yesu kuna umuhimu gani kwetu? Andaa sala ya shukrani kwa yote ambayo Mungu aliyafanya kwa kumtuma Mwanae. ***2 Wakorintho 9: 15*** |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Umejifunza nini kutokana na funzo hili?<br>2. Je! Unafikiri malaika wanaonekana leo? Kwanini wanaonekana / kwanini hawaonekani? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je! Mungu amewahi kukuambia au kumwambia mtu unayemjua kuhusu kitu ambacho kilikuwa vigumu kukiamini?<br>2. Je! Ni unabii gani ambao tumesoma katika Maandiko ya Biblia kwa ajili ya funzo hili ambao ulitimia wakati ambapo Bwana Yesu alikuja? Taja zaidi ya moja. |

| | **A12 – DARAJA LA 3**<br>**Somo la Pili – Krismasi ya Kwanza**<br>**Mada – Kazi Maalum** | **A12 – DARAJA LA 4**<br>**Funzo la Pili – Kuzaliwa kwa Mwokozi**<br>**Mada – Amri ya Mfalme** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Luka 1: 26-38***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 1: 38***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mariamu na Yusufu walikuwa wanandoa wa kipekee, ambao Mungu aliwatumia kwa namna ya ajabu.<br>2. Kuzaliwa kwa Yesu, Mwana wa Mungu, kulikuwa ni muujiza. | **Neno la Biblia:** ***Luka 2: 1-7***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 2: 7***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Utawala wa Rumi ulikuwa na watawala walioitwa Kaisari.<br>2. Kaisari alitoa amri ambayo ilimaanisha kwamba Mariamu na Yusufu walipaswa kwenda Bethlehemu kujisajili. Hili lilitimiza unabii wa Agano la Kale. |
| **TOA UTANGULIZI** | Fikiria juu ya uhalisia kwamba mojawapo ya mambo ya kwanza kufanya mtoto anapozaliwa ni kumpatia mtoto jina. Yesu ana majina au vyeo vingi. Angalia kupitia maelezo ya kuzaliwa kwa Yesu katika ***Luka 1 na 2, na Mathayo 1 na 2*** na orodhesha baadhi ya majina Yake na vyeo Vyake. Unapenda zaidi jina au cheo kipi na kwa nini? | Katika vikundi vidogo andika majina ya maeneo mengi kadri uwezavyo ambayo yametajwa katika Maandiko ya Biblia kwenye Funzo hili. Fanya hivyohivyo kwa majina ya watu. Angalia majibu yako kwa kusoma tena Maandiko haya ya Biblia. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Pengine Mariamu ni msichana mdogo aliyechumbiwa na Yusufu.<br>2. Anatembelewa na malaika Gabrieli na anasumbuka anaposikia kwamba Mungu amempa neema kubwa.<br>3. Malaika anamwambia atajifungua mtoto ambaye jina lake litakuwa Yesu. Yeye ni Mwana wa Aliye Juu na atampa kiti cha enzi cha baba yake Daudi.<br>4. Mariamu anachanganyikiwa kwa kuwa bado ni bikira lakini malaika anafafanua kuwa atachukua mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.<br>5. Mwitikio wa Mariamu ni wa kushangaza sana, anasema, "Na iwe kwangu kama ulivyosema"<br>6. *Fikiria mambo mbalimbali ambayo unadhani yalikuwa yakiendelea kichwani kwa Mariamu wakati malaika alipomwambia amepewa neema kubwa na atachukua mimba. Tazama pia* ***mistari ya 46 & 47.***<br>7. *"Hakuna lisilowezekana kwa Mungu." Fikiria kuhusu watoto wengine kwenye Biblia ambao walizaliwa katika mazingira yasiyowezekana kibinadamu.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – The birth of Jesus (P & I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Wote Mariamu na Yusufu walikuwa uzao wa Mfalme Daudi, na kwa hivyo wakati amri ilipotolewa kwa ajili ya sensa, walilazimika kwenda Bethlehemu.<br>2. Ilikuwa takriban maili 70 na safari ngumu sana kwa Mariamu ambaye alikuwa karibu kujifungua. Inawezekana Bethlehemu kulikuwa na watu wengi kwa hivyo walilazimika kukaa pengine katika aina fulani ya zizi au pango.<br>3. Hapa Yesu alizaliwa katika mazingira duni, ya hali ya chini.<br>4. Fikiria juu ya mambo kadhaa ambayo yalipaswa kutokea ili Yesu azaliwe huko Bethlehemu kama vile Mika alivyokuwa amesema, na ushangazwe na nguvu ya Mungu ya kufanya haya yote yatimie. ***(Mika 5: 2)***<br>5. Soma ***Yohana 3:16, na Wagalatia 4: 4*** na ufikirie kuhusu maana ya mistari hii katika kumsaidia kila mtu kuelewa tukio hili kuu.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – The birth of Jesus (P & I)** |
| **REJELEA SOMO** | **Jibu haya maswali:**<br>1. Huyu malaika aliitwa nani?<br>2. Mwitikio wa kwanza wa Mariamu kuhusu habari hii ulikuwaje?<br>3. Mariamu alijisikiaje baada ya muda fulani kupita? (tazama ***mistari ya 46 & 47***) | **Jibu haya maswali:**<br>1. Taja mji au jiji ambalo liko takriban umbali wa maili 70 kutoka hapo unakoishi.<br>2. Wanafunzi wangekuwa tayari kutembea umbali huo, hata bila kuwa wajawazito?<br>3. Ni nini kilikuwa cha tofauti kuhusu mazingira ya kuzaliwa kwa Yesu ikilinganishwa na kuzaliwa kwa watoto siku za leo? |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Katika vikundi vidogo andika jina la maeneo yote yaliyotajwa katika kifungu hiki cha Biblia, halafu fanya vivyo hivyo kwa majina ya watu. Hakiki uone kama umeruka au kuacha lolote kwa kusoma tena kifungu hicho cha Biblia.<br>Fikiria juu ya umuhimu wa kila kitu ambacho kimeandikwa. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Andika insha kwa mtazamo wa Yusufu yenye kichwa: "Mariamu mjamzito wa karibu kujifungua alisafiri maili 70 kabla ya kujifungua mtoto wetu ambaye alilazwa katika hori." |

| | **A12 – DARAJA LA 3**<br>**Somo la Tatu – Krismasi ya Kwanza**<br>**Mada – Huko Bethlehemu** | **A12 – DARAJA LA 4**<br>**Funzo la Tatu – Kuzaliwa kwa Mwokozi**<br>**Mada – Ziara ya Wachungaji** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Luka 2: 1-20***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 2: 11***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ilikuwa mpango wa Mungu kwamba Yesu azaliwe katika hali duni na ngumu.<br>2. Mungu alikuwa akidhibiti yote yaliyotokea na hata leo anafanya hivyo. | **Neno la Biblia:** ***Luka 2: 8-20***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 2: 11***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Malaika aliwatokea wachungaji walipokuwa wakiendelea kufanya shughuli zao za kila siku.<br>2. Waliamini kile walichosikia na kuchukua hatua za haraka. |
| **TOA UTANGULIZI** | Waambie wanafunzi wataje matukio makubwa zaidi kwenye historia. Eleza kwamba kuja kwa Mwana wa Mungu lilikuwa ni tukio kubwa. Chora ratiba ya nyakati inayoonesha matukio yote ya kifungu hiki. | Katika vikundi vidogo badilisha kifungu hiki kuwa mchezo wa kuigiza. Tumia vitendea kazi rahisi kama vile mitandio au vitambaa vyovyote kwa ajili ya skafu za mchungaji. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Wote Mariamu na Yusufu walikuwa uzao wa Mfalme Daudi kwa hivyo wakati amri ilipotolewa kwa ajili sensa, walilazimika kwenda Bethlehemu.<br>2. Hii ilikuwa takriban maili 70 na safari ngumu sana kwa Mariamu ambaye alikuwa karibu kujifungua.<br>3. Bethlehemu ilikuwa na watu wengi kwa hivyo walilazimika kukaa labda katika aina fulani ya zizi au pango. Hapa Yesu alizaliwa katika mazingira duni na ya hali ya chini.<br>4. Tunadhani kuzaliwa kwa Yesu kulitokea usiku na wachungaji walikuwa baadhi ya watu wachache waliokuwa macho/ hawajalala.<br>5. Walipokea habari ya kuzaliwa kwa Mwokozi - Kristo Bwana.<br>6. Kundi kubwa la jeshi la mbinguni liliwatokea wachungaji likimsifu Mungu.<br>7. Wachungaji waliamua kwenda Bethlehemu na kuona kilichokuwa kimetokea. Walimkuta Mariamu na Yusufu na Mtoto.<br>8. Walieneza habari ya yote waliyoyaona na kisha wakarudi wakimsifu na kumtukuza Mungu.<br>9. *Fikiria salamu ya kwanza malaika waliyotoa kama ilivyoandikwa hapa na mahali pengine katika Biblia.*<br>10. *Fikiria kuhusu jinsi ambavyo wanandoa hawa wachanga walijihisi kwenye safari yao.*<br>11. *Jadili masomo ambayo tunaweza kujifunza kutoka kwenye habari ya wachungaji.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Shepherds hear the birth of Jesus (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Tunadhania kuzaliwa kwa Yesu kulitokea usiku na wachungaji walikuwa baadhi ya watu wachache waliokuwa macho/hawajalala.<br>2. Walipokea habari ya kuzaliwa kwa Mwokozi - Kristo Bwana.<br>3. Kundi kubwa la jeshi la mbinguni liliwatokea wachungaji likimsifu Mungu.<br>4. Wachungaji waliamua kwenda Bethlehemu na kuona kilichokuwa kimetokea. Wakamkuta Mariamu na Yusufu na Mtoto, kama vile walivyoambiwa.<br>5. Walieneza habari ya yote waliyoyaona na kisha wakarudi wakimsifu na kumtukuza Mungu.<br>6. *Fikiria kuwa Mungu alionekana kwa watu hawa kupitia kwa malaika walipokuwa wanafanya kazi. Anaweza kuongea nasi leo tukiendelea na maisha yetu ya kila siku.*<br>7. Tunaposikia juu ya yale ambayo Mungu ametufanyia tunapaswa kuwaambia wengine.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Shepherds hear the birth of Jesus (I)** |
| **REJELEA SOMO** | **Jibu haya maswali.**<br>1. Je! Unafikiria ni kwanini malaika wanawasalimu watu kama kwenye ***mstari wa 10?***<br>2. Je! Unadhani Mungu bado anasema leo na watu wa kawaida kama wachungaji kupitia kwa malaika? Kwanini anafanya hivyo / kwanini hafanyi hivyo?<br>3. Je! Unafikiria nini kilikuwa kwenye akili ya Mariamu? ***(Mstari wa 19)*** | **Jibu haya maswali.**<br>1. Je! Unafikiri kwanini wachungaji walichukua hatua ya haraka mara tu malaika alipoondoka?<br>2. Wachungaji walibarikiwa kwa hatua yao ya haraka. Je! Unaweza kuuandika ***mstari wa 20*** katika maneno ya siku hizi?<br>3. Je! Unafikiria nini kilikuwa kwenye akili ya Mariamu? ***(Mstari wa 19)*** |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Jifanye kama ulikuwa mchungaji. Kwa kutumia ***mstari wa 8-17*** andika kwenye kitabu chako cha kumbukumbu ukielezea kile ulichosikia, kuona na kuhisi. | Zingatia kutunza kumbukumbu ya mambo ambayo Mungu anasema na wewe na tarehe ili uweze kurejelea na kutiwa moyo kwa mambo ambayo Mungu anafanya katika maisha yako. |

| | A12 – DARAJA LA 3<br>**Somo la Nne – Krismasi ya Kwanza**<br>**Mada – Hekaluni** | A12 – DARAJA LA 4<br>**Funzo la Nne – Kuzaliwa kwa Mwokozi**<br>**Mada – Zawadi za Mamajusi** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Luka 2: 22-40***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 2: 30***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Simeoni na Ana walifurahia kuzaliwa kwa Yesu kwa sababu walielewa umuhimu wake.<br>2. Ni muhimu kumshukuru Mungu kwa kumtuma Yesu ulimwenguni. | **Neno la Biblia:** ***Mathayo 2: 1-23***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 2: 11***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ingawa mamajusi walileta hazina, Yesu alikuwa hazina ya kweli.<br>2. Wanaume hawa walielewa kuwa Yesu alikuwa mtu wa pekee sana. |
| **TOA UTANGULIZI** | Fikiria kuhusu furaha inayokuwepo wakati mtoto anapozaliwa. Kitu gani kilikuwa cha tofauti kuhusu kuzaliwa kwa Yesu? Elezea kwamba sheria za Kiyahudi zilikuwa kwamba wazazi wanatakiwa kwenda Hekaluni ili kumpa mtoto jina, kumtahiri, na kutoa sadaka kwa ajili ya utakaso wa mama na kumshukuru Mungu. ***(Mambo ya Walawi 15)*** | Fikiria kuhusu furaha inayokuwepo wakati mtoto anapozaliwa. Fikiria kuhusu familia na marafiki wakisafiri kwa ajili ya kumuona mtoto mchanga. Watambulishe mamajuzi na safari ndefu waliyoifanya.<br>Fikiria jinsi ambavyo katika habari hii Mungu alikuwa yuko mbele ya Shetani siku zote. Orodhesha mifano kutoka kwenye kifungu hiki. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Baada ya Yesu kuzaliwa, anapelekwa Hekaluni huko Yerusalemu.<br>2. Mariamu na Yusufu, wote walikuwa wameambiwa kuhusu kumpa jina mtoto Yesu na hili ndio walilofanya! Sasa walitoa dhabihu kama Sheria ilivyowaamuru.<br>3. Walikutana na Simeoni ambaye alikuwa ameambiwa kwamba hatakufa mpaka atakapomuona "Kristo wa Bwana".<br>4. Alimpokea mtoto mikononi mwake na akamsifu Mungu kwa sababu alitambua kuwa Yesu alikuwa ni Mwokozi.<br>5. Pia walikutana na mwanamke mzee anayeitwa Ana, ambaye pia alimshukuru Mungu na "alizungumza juu ya Mtoto huyo kwa wote wanaotazamia ukombozi wa Yerusalemu."<br>6. *Fikiria jinsi ambavyo Simeoni na Ana walijua kwamba Yesu alikuwa mtu wa pekee.*<br>7. *Fikiria kuhusu mambo ambayo waliyasema kwamba yangetokea kwa Yesu.* ***(tazama mistari 31-31, 34, 35, na 38)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Simeon and Anna meet Baby Jesus (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mamajusi waliona nyota upande wa Mashariki na kutokana na elimu yao walitambua kuwa mfalme mpya alikuwa amezaliwa na walitaka kumtembelea ili kumsujudia.<br>2. Walimtembelea Herode katika Ikulu ya Yerusalemu, wakidhani mfalme mpya atakuwa huko.<br>3. Herode inafadhaika, akidhani amepata mpinzani bali kupitia kwa watu wa dini anaambiwa kuhusu ***Mika 5: 2*** na kuzaliwa kwa Mfalme huko Bethlehemu.<br>4. Mamajusi wanaenda Bethlehemu, wanamkuta Mtoto, wanampa hazina zao na kumwabudu.<br>5. Wanaonywa katika ndoto kurudi nyumbani kwa njia nyingine na wasimwambie Herode nini walichokuwa wameona.<br>6. Yusufu anaambiwa amchukue Mariamu na Mtoto waende Misri kwa ajili ya usalama.<br>7. Herode anatambua kwamba amedanganywa kwa werevu na kutoa maagizo ya kuuawa kwa wavulana wote wa Bethlehemu wenye umri chini ya miaka miwili.<br>8. Hatimaye Yusufu anaambiwa ni salama kurudi na kuishi Nazareti.<br>9. *Fikiria jinsi Mungu alivyokuwa amepanga haya mamia ya miaka kabla ya unabii mbalimbali kutimia.* ***(Angalia mistari 5-6, 15, 17-18, na 23)***<br>10. *Pia fikiria jinsi Herode alivyokuwa anafanya kazi ya Shetani.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Wise men visit and worship Jesus (I & P)** |
| **REJELEA SOMO** | Simeoni alisema kuwa atakuwa Nuru. Katika vikundi vidogo/ vya watu wawiliwawili, fikiria kuhusu vitu vyote vizuri ambavyo nuru huvifanya. Ni kwa njia zipi wanaweza kuona ***mstari wa 32*** kwa namna ya tofauti kidogo sasa? Wape wanafunzi changamoto waombe kwamba Mungu atume nuru Yake zaidi katika maisha yao. Wahamasishe wafikirie kuhusu maeneo maalum ambayo wanahitaji msaada na kugeuza mambo haya kuwa sala. | Fikiria zawadi ambazo alipewa Yesu- Dhahabu ikimaanisha kuwa yeye ni Mfalme, Manemane ikimaanisha kuwa Yeye ni Mwokozi ambaye atateseka na kufa, na Uvumba ukiwakilisha kuwa Yeye ndiye Mungu ambaye tunamwabudu.<br>Fikiria njia zote ambazo Yesu ni kama hazina, zawadi ya bure kwa mtu yeyote ambaye atampokea kama Mwokozi na Bwana. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Mambo gani tunaweza kujifunza na kuyatumia katika maisha yetu kutokana na somo hili?<br>2. Kumbuka kuwa wokovu una maana ya ukamilifu wa mambo yote na sio tukio la mara moja tu bali ni mchakato wa maisha yote. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Fikiria kuhusu kitu tunachoweza kumletea Bwana Yesu kama sadaka.<br>2. Orodhesha mifano fulani ya kila siku / habari ya kweli ambapo Shetani ni 'Mdanganyifu.' Kuwa makini kwa jinsi anavyotenda kazi. |

## Maelekezo ya waalimu wanaposahihisha masomo

**Masomo ya Daraja la Tatu**

- Wanafunzi hawawezi kukamilisha masomo haya bila kurejelea Biblia na wanaweza kulazimika kurejelea kifungu kimoja au zaidi vya Maandiko ya Biblia.
- Maswali yapo katika namna mbalimbali ikiwa ni pamoja na jedwali la maneno, maneno yaliyokosekana, n.k.
- Masomo yametegenezwa kujibiwa kwa toleo la Biblia ya Kiswahili, Union Version iliyochapishwa kama "BIBLIA Maandiko Matakatifu".
- Lengo letu ni kwamba wanafunzi wote, waweze kujibu maswali kwa kutumia Biblia yoyote waliyo nayo.
- Alama ishirini zimetengwa kwa kila wiki ambapo kiwango cha juu kwa mwezi ni 80, pale masomo yanapokuwa ni sahihi kabisa.
- Daraja la tatu – Kwa kawaida na kama inavyooneshwa, alama 1 kwa kila jibu linalohitajika.

**Mafunzo ya Daraja la Nne**

- Masomo haya ni ya ngazi ya juu ya yale masomo ya Daraja la Tatu.
- Maswali ni ya kiwango cha juu na majibu ya kina zaidi yanahitajika.
- Alama ishirini kwa wiki na alama 80 kwa mwezi, wakati masomo yakiwa ni sahihi kabisa na maswali yana majibu kamili.

**VIDOKEZO VYA KUSAHIHISHA**

Walimu wanatakiwa, kwanza:

- Kukagua vizuri kila somo na kusahihisha majibu yaliyo sahihi au yasiyo sahihi.
- Toa alama kama ilivyoelekezwa.
- Kila mara, tumia kalamu ya rangi tofauti kusahihisha na kuweka ALAMA YA VEMA (✔) kwenye kila jibu sahihi.
- Weka au andika jibu sahihi panapostahili, na rekebisha makosa yoyote ya maandishi (spelling errors), lakini HAKUNA alama zinazoondolewa kwa ajili ya kosa hili.
- Toa alama chache kwa kila jibu ambalo sio sahihi kabisa.
- Jumlisha alama za mwezi na uandike kwenye nafasi iliyotolewa kwenye ukurasa wa mwisho.

Ni muhimu kuwa mkarimu kama uwezavyo ili kuwatia moyo watoto/ wanafunzi wafanye masomo ya Biblia. Kila mwezi, ni muhimu kwa mwalimu kuandika maneno ya kutia moyo kwenye nafasi iliyowekwa kwa kila mtoto anayemfundisha. Unaweza kuandika kuhusu kupaka rangi vizuri, kufanya kazi safi, alama alizopata mtoto, uelewa wa masomo wa mtoto na kadhalika.
Tunajaribu kutoa mawazo tofauti kama iwezekanavyo. Maswali, maoni, maneno ya kutia moyo na kadhalika, yote yanaweza kutumiwa kuleta utofauti. Kama maoni au usemi mmoja unatumika kila mwezi, watoto watauona hauna maana tena.

**Daraja la Tatu**
**Maoni ya jumla**

"Kazi njema! Ni wazi kwamba umesoma maswali kwa umakini sana. Nilipenda sana jibu lako la swali la mwisho ambalo lilikuwa limeandikwa vizuri. "
"Habari Yusufu. Hongera kwa kufanya kazi kwa bidii sana! Ilikuwa vizuri kwamba uliweza kujibu takriban majibu yote. Nimekujazia yale ambayo hayajakamilika."

**Maoni ya kiroho**

"Musa alikuwa na wakati mgumu na wana wa Israeli, lakini Mungu hakumwacha kutatua matatizo yote peke yake."
"Yusufu hakusahau kuwa baba yake alikuwa amemfundisha kumpenda Mungu. Alikumbuka hili hata alipokuwa mbali na nyumbani."
"Bartimayo alikuwa ameazimia kufika kwa Bwana Yesu. Hakujutia uamuzi wake kwani sasa alikuwa na uwezo wa kuona na sasa alijua kuwa Bwana Yesu alikuwa mtu wa pekee sana."

**Daraja la Nne.**
**Maoni ya jumla**

"Seti nyingine nzuri sana ya masomo. Unaonekana kuwa na ufahamu mzuri wa habari hizi za Biblia na ninatumaini kuwa umezifurahia. Asante kwa kutumia muda wako kufanya masomo kwa umakini. Ungeliweza kufanya masomo haya kwa haraka haraka, kwahiyo ninathamini juhudi zako zote."
"Neema, umejitahidi sana. Nadhani kwa majibu uliyoyatoa, pengine haukuweza kuelewa habari vizuri. Labda ungejaribu kuisoma tena."

**Maoni ya kiroho**

"Mifano ya Biblia wakati mwingine huitwa habari za kidunia zenye maana ya kimbingu, au maana ya ndani zaidi. Je! Unaweza kufikiria kuna maana gani ya kina katika mfano kwenye Funzo la Tatu?"
"Stefano alikufa kifo cha kikatili na bado hakuogopa kufa, kwa vile alijua kuwa Mungu bado anatawala kila jambo na alijua atakuwa na Bwana Yesu Mbinguni."

© Bible Educational Services 2019

www.besweb.com

Registered Charity UK 1186004

Toleo la 11/2020